# Kuwalea watoto kwa utukufu wa Mungu

## Edward Payson (1783-1827)

*“Binti Farao akamwambia, Mchukue mtoto huyu, ukaninyonyeshee, nami nitakupa mshahara wako” (Kutoka 2:9).*

Maneno haya yalizungumzwa na Binti wa Farao kwa mama wa Musa. Musa alizaliwa wakati ambapo Farao wa Misri alikuwa ametoa amri kwamba watoto wa kiume wa Waisraeli walikuwa wote wauliwe. Kwa sababu mama yake Musa hakuwa tayari kumwua mwanawe, alimficha ndani ya kikapu ambacho alikuwa amekipaka lami na akakiweka juu ya maji ya mto naili ambapo Binti ya Farao alimpta. Wakati Binti ya farao alimpata, alifurahi sana kiwango kwamba hakuwa tu tayari kumwokoa, bali pia alikuwa tayari kumchukua kama mtoto wake. Dada yake Musa ambaye aliitwa Mariamu yeye alikuwa amesimama kwa ubali akitaza kuona nini ambacho kingemfanyikia ndugu yake. Wakati aliposikia maneno ya Binti Farao kwamba alihitaji mtu wa kumlelea mtoto Musa, alijitolea kumtafutia mtu ambaye alikuwa mama yake. Wakati Binti wa farao alikubali wazo la dadake Musa, dadake Musa alikimbia na kumwita mamake. Binti wa Farao alimwamibia mama ya Musa, “mchukue mtoto huyu, ukaninyonyeshee, name nitakupa msahara wako.”

Kwa njii hiyo hiyo, Mungu anazungumza na kila mzazi. Kwa wale ambao Mungu amewabarikiwa na watoto, wakati Mungu alikuwa akikupatia mtoto huyo, alisema maneno haya kwako, “Mchukue mtoto huyu, ukaninyonyeshee, name nitakupa mshahara wako.” Kutokana na maneno haya, ninataka kukuonyesha inamaanishi nini kuchukua mtoto na kumnyonyesha au kumlea kwa utukufu wa Mungu.

Kuna mambo manne ambayo tutatazama kutokana na mstari huu wa Kutoka 2:9.

### I. Kwanza, ikiwa tutawalea watoto wetu kwa utukufu wa Mungu, ni lazima tufahamu kwamba watoto ni wa Mungu, wao ni mali Yake.

Mungu huwa anatupatia watoto hawa kwa muda ilituweze kuwalea na kuwafundisha kuhus Mungu, kama tu sisi wenyewe tunavyowapatiana kwa walimu katika mashule kuwafundisha mambo ya elimu. Ukweli ni kwamba, ikiwa hatutatambua kwamba watoto wetu ni mali ya Mungu, basi hatutaweza kuwalea na kuwafundishi kwa ajili ya utukufu wa Mungu. Tunaweza kuonekana kwamba tuwapatia kile ambacho ni kizuri sana na kwamba nia zetu ni nzuri juu ya maisha yao. Lakini ikiwa kulea kwetu hakutokana na kumtambua Mungu kwamba Yeye ndiye mwenye watoto wetu, kamwe hatutakuwa tunatekeleza majukumu yetu sawasawa, kwani tutakuwa tunawalea kwa utukufu wetu na wala si wa Mungu.

Kujua kwamba watoto ni Mungu, ni kufahamu kwamba Mungu ana nguvu za kufanya nao jinsi anavyotaka hata kuwatowa kwetu milele. Kuna msitari mingi sana katika Biblia ambayo indhihirisha jambo hili kwamba watoto ni wa Mungu. Biblia inafundisha kwamba, Mungu ndiye ametuumba na kwamba Yeye ndiye Baba wa nafsi zetu na sisi ni mali yake na wala si mali yetu wenyewe. Biblia inasema kwamba nafsi ya mzazi na ile ya mwanawe, zote ni za Mungu (Ezekiel 18:4). Mungu aliwakemea na kuwaadhibu sana Wayahudi kwa sababu waliwatoa watoto wao kama sadaka kwa moleki ambye alikuwa sanamu (Ezekieli 16:20-21).

Wengi wa wazazi huwa hawa, hawatilii manaani jukumu hili. Wengi huwa hawazingatii ukweli kwamba wao na watoto wao, ni mali ya Mungu, na kwamba wao kama wazazi, wamepewa tu jukumu la kulea kwa utukufu wa Mungu. Mungu amewapatia mali yake ili waweze kuitunza sasa kulingana na mapenzi yake. Ikiwa mzazi yeyote hatawaza hivi kwamba watoto wake, ni mali ya Mungu, basi mzazi huyu hataweza kuwalea watoto hao kwa utukufu wa Mungu. Itakuwa vigumu sana kwao kuwalea watoto kwa utukufu wa Mungu ambaye wao wamemkata kwamba yeye si mwenye watoto wao; yaani watoto wao si mali ya Mungu.

### II. Pili, ikiwa tutawalea watoto wetu kwa utukufu wa Mungu, ni lazima tuwapatiane kwa Mungu milele.

Tumeona kwamba watoto wetu ni mali ya Mungu na wala si mali yetu. Kupatiana watoto kwa Mungu inamaanisha kumtambua Mungu na neno lake. Ni kujua kwamba kweli watoto wetu ni mali yake na kwamba sisi ni vyombo vyake Mungu ambavyo anatumia kutekeleza mapenzi yake katika maisha ya watoto wetu. Inamaanish kuwalea tukikumbuka kwamba wao ni mali yake sasa na ahata milele. Ikiwa

hatutawapatiana kwa Mungu, ni wazi kwamba hatutakuwa tunawalea kwa utukufu na sifa kwa Mungu.

### III. Tatu, ikiwa tutawalea watoto wetu kwa utukufu wa Mungu, ni lazima tuhakikishe kwamba yale ambayo tunawafanyia watoto wetu yawe ni kwa utukufu wa Mungu.

Biblia inafundisha kwamba ikiwa kusudi letu la kufanya jambo lolote si kwa utukufu wa Mungu, au kuendeleza mapenzi na mipango yake, basi hatutakuwa tunafanya chochote kwa ajili ya Mungu. Chochote ambacho hakitokani na kumletea Mungu utukufu, si cha Mungu.

Kwa hivyo tunapaswa kuongozwa na ukweli huu katika majukumu yetu ya kuwalea watoto wetu ikiwa kweli tutakuwa tunawalea kwa ajili ya utukufu wa Mungu na si kwa ajili yetu. Katika hali zote, taabu na furaha wakati tunawalea watoto wetu, lazima tukumbuke kumletea Mungu utukufu. Ikiwa tutawalea watoto wetu kwa sababu tunawapenda sana na kwamba tunataka wawe watu fulani katika maisha yao na kupuuza utukufu wa Mungu, basi hatutakuwa tofauti na wanyama ambao huwalea watoto wao na wakishafika umri fulani wao huwasahau. Lakini ikiwa majukumu ya wazazi kwa watoto wao yatakuwa yanaelekezwa na upendo na sifa kwa Mungu, basi ni kweli kwamba tutakuwa tunawalea watoto wetu kwa utukufu wa Mungu na si kwa utukufu wetu.

Ukristo wa kweli huwa unamletea Mungu utukufu na sifa. Ukristo wa kweli huwa kila wakati, katika kila jambo, hutafuta Mungu utukuzwe. Kwa hivyo hata kama kazi ya kuwalea watoto huwa inaonekana kuwa jambo gumu na wengi, lazima tuifanye kwa utukufu wa Mungu. Ikiwa tutawalea watoto wetu kwa ajili ya kumletea Mungu utukufu, basi tutakuwa tuinadhihirisha ukristo wa kweli.

### IV. Nne, ikiwa tutawalea watoto wetu kwa utukufu wa Mungu, ni lazima tuwafundishe kumtumikia Mungu.

Mambo matatu ya kwanza ambayo tumeyaona, yanazungumzia sana, majukumu yetu  na nia zetu. Hili jambo la nne, linahusu sana watoto wetu. Ikiwa kweli tunaweza kuwalea watoto wetu kwa njia ambayo inamletea Mungu sifa na kuwatayarisha kwa ajili ya kumtumikia Mungu, basi ni wazi kwamba lazima tusome, tujifunze na tutii neno la Mungu. Pia lazima tuombe Roho Mtakatifu kwamba atatusiadia na pia awasaidie watoto wetu kuelewa na kutii neon la Mungu. Ni lazima tuhakikishe kwamba hatufanyi lolote ambalo litawafanya wadharau neno la Mungu. Tuhakikishe kwamba sisi wenyewe tunakuwa mfano

mwema wa maisha ya ukristo kwa watoto wetu. Ni lazima tuhakikishe kila wakati kwamba tunawafundisha neno la Mungu na kuwaonyesha kwamba hakuna kitu cha mihumu zaidi katika maisha haya isipokuwa kuishi maisha yetu kwa utukufu wa Mungu. Pia lazima tuwaonyesha kwamba furaha ya kweli, inatokana na kumwamini Kristo. Ni lazima tuwajulishe kwamba hakuna jambo lingine la muhimu katika maisha ya mtu isipokuwa kuishi maisha yake akiwa ndani ya Kristo.

# KUWALEA WATOTO KATIKA ADABU NA MAONYO YA BWANA

## David Martyn Lloyd-Jones (1899-1981)

*"Nanyi akina baba, msiwachokoze watoto wenu; bali waleeni katika adabu na maonyo ya Bwana" (Waefeso 6:4).*

Ikiwa tutaweza kufanya kile ambacho Biblia inasema katika mstari huu, lazima kwanza tujua nini tunapaswa kufanya ili tuweze kutekeleza jukumu hili. Kila wakati mtu anapopata mtoto anapaswa kufahamu kwamba amepata jukumu la kuongoza nafsi ya mtoto huyo. Hili ni jukumu kubwa sana ambalo halifai kupuuzwa hata kidogo. Katika biashara wenye biashara huwa wanajua majukumu ambayo wako nayo katika uamuzi ambao wanapaswa kutoa kwa ajili ya kunawili kwa biashara zao. Ni jambo la kuhuzunisha kwamba hata kama wengi wanashughulika sana na biashara, wao husahau majukumu yao makubwa juu ya watoto wao. Wao wanamaliza muda wao mwingi katika mambo mengine na wanasahau kuwalea watoto wao katika adabu na maonyo ya Bwana. Mwandishi wa kitabu cha Waefeso anataka tujue kwamba ni jukumu kubwa na la maana sana katika maisha ya kila mzazi kuwalea watoto wake katika adabu na maonyo ya Bwana.

Mwandishi anasema kwamba tuwalee watoto wetu katika adabu na maonyo ya Bwana. Maneno haya yote ni ya muhimu sana. Wakati anaposema waleeni, hili ni jambo la kawaida kwa kila mzazi na wengi watasema kwamba hiyo tunajua. Waleeni ni neno ambalo linajumlisha kila kitu ambacho tunawafanyia watoto wetu kama kuwapa chakula,

mavazi na kuwapeleka shuleni. Lakini mwandishi anazungumza zaidi kwa kutueleza jinsi tunapaswa kuwalee watotot wetu. Neno adabu nalo linahusu kuwalea watoto katika tabia mzuri na kuwasaidia kujifahamu na kujua jinsi wanapaswa kuishi katika maisha haya. Kwa ufupi inammanisha kuwalinda watoto na kuwatunza watoto wetu.

Kuna mambo mawili kuhusu jambo la adabu, Kwanza tunahitaji kushughulika na tabia ya watoto wetu na halafu kuna haja ya kuwafundisha. Ni lazima tuwaambie maneno ya kuwahimiza, maneno ya kuwakemea na maneno ya kuwaonyesha kuajibika katika maisha yao. Hii ndio maana halisi ya neno adabu.

Watoto lazima tuwalee katika adabu na maonyo ya Bwana. Wakati biblia inasema katika maonyo ya Bwana, inamfanya mzazi ambaye ameokoka awe tofauti kabisa na yule mzazi ambaye hajaokoka. Maneno haya kwa wazazi ambao wameokoka situ kuwaonyesha watoto jinsi ya kuwa watu wenye tabia mzuri, wenye kuwaheshimu wengine na wenye kujukumika katika maisha yao, kwa sababu hata wale wote ambao hawajaokoka haya ni mambo ambayo wanawafundisha watoto wao. Kwa kawaida hakuna mzazi ambaye angependa mtoto wake akue akiwa na tabia ambazo ni mbaya. Kila mtu anataka mtoto wake awe na tabia mzuri ambazo wengi wanatamani. Mzazi ambaye ameokoka jukumu lake ni zaida ya tabia mzuri, kwani anaambiwa katika neno la Mungu kwamba awalee watoto wake katika adabu na maonyo ya Bwana.

Hii inamaanisha kwamba wazazi ambao tumeokoka lazima tuwalee watoto wetu katika kumfahamu Yesu Kristo kama Bwana na Mwokozi. Hili ni jukumu la kila mzazi ambaye ameokoka, kuhakikisha kwamba watoto wake wanajua njia ya wokovu jinsi Biblia inavyofundisha. Hili si jukumu lao tu, bali inafaa kuwa tamaa ya mioyo yao kwamba watoto wao wanaokoka. Je, hii ni tamaa juu ya maisha ya watoto wako? Je, katika mipangilio yako yote kuwahusu watoto wako, je wao kumjua Kristo ni tamaa na kusudi lako la kwanza? Je, wewe unatamani kwamba watoto wako waokoke au la? Kuwaongoza watoto wako ili waokoke, ndio maana ya adabu na maonyo ya Bwana.

Biblia inasisitiza sana kuhusu kuwalea watoto katika adabu na maonyo ya Bwana. Kwa mfano katika Kumbukumbu la Torati 6, tunasoma wakati Musa alikuwa amekaribia kufa na Waisreali walikuwa karibu kuingia katika nchi ya Kanani. Yeye Musa aliwakumbusha kuhusu sheria ya Mungu na kuwaelezea jinsi walipaswa kuishi maisha yao katika nchi ya Kanani. Miongoni mwa mambo mengine yote, aliwasihi kwamba walihitaji kuwafundisha watoto wao sheria ya Mungu. Haikutosha tu kwamba wao waliijua na kutii, bali pia

walihitaji kuwaeleza watoto wao kuhusu sheria hiyo. Walihitaji kuwafundisha watoto wao na wasisahau.

Hili jambo la kuwalea watoto katika adabu na maonyo ya Bwana ni jambo ambalo wakristo wengi hata katika historia wamelitilia mkazo sana. Wao wamekuwa waangalifu sana jinsi wamewalea watoto wao kwa utukufu wa Mungu. Kwa sababu ya umuhimu wa jambo hili, mahubiri mengi yamehubiriwa na vitabu vingi vimeandikwa kuhusu jambo hili.

Wakati mtu anaokoka, kazi ya wokovu huwa inaleta badiliko makubwa sana maishani mwa mtu. Mtu ambaye ameokoka, hawezi akaishi maisha yake kama yule ambaye hajaokoka. Wokovu ni kazi ya Mungu ambayo huwa inabadilisha kila sehemu ya maisha ya yule ambaye ameokoka. Huwa inabadilisha maisha yake katika ndoa na katika jamii yake kwa ujumla. Unapotazama ndoa za wale ambao wameokoka, utaona kwamba ni wachache sana ambao wanapeana talaka ikilinganishwa na wale ambao hawajaokoka. Kazi ya wokovu pia huwa inabadilisha maisha katika jamii. Utaona kwamba wale ambao wameokoa wanawalea watoto wao kwa kusudi moja, utukuf wa Mungu. Wakati wale ambao wameokoka wanaishi maisha yao kwa njia ambayo inamletea Mungu sifa, huwa wanashawishi wengi kwa njia ya maisha yao kuju kwa Kristo Yesu na hata wale ambao wanakataa kuokoka, huwa maisha yao inabadilika hata kama si kwa kuja kwa Kristo Yesu.

Kwa ufupi ni kwamba hakuna njia nyingine ya kuleta badiliko katika jamii isipokuwa kwa nguvu za Injili ya Yesu Kristo. Hakuna ukweli bila wokovu. Watu wanapookoka, wao huendelea katika maisha yao yote kuishi maisha ya ukristo na pole pole hata wengi wanaendelea kubadilika kwa kuwa wale ambao wameokoka wanaonyesha mfano mwema katika maisha yao. Ikiwa wote ambao tumeokoka, tutaishi maisha matakatifu, basi ni wazi kwamba tutaona wengi wakibadilika na kuja kwa Kristo. Ni jambo la kuhuzunisha kwamba wengi ambao wameokoka, hawaishi maisha yao kwa njia ambayo inamletea Mungu utukufu. Jamii nyingi ambazo zinadai kujua Kristo, hawatilii maanani, kuishi maisha yao kulingana na neno la Mungu. Leo hatuoni wengi wakijitahidi katika utakatifu. Leo unapotazama mahali kwingi utapata kwamba wengi hawatilii maanani majukumu yao ya kuwalea watoto wao katika adabu na maonyo ya Bwana. Wengi wanapuuza jamii zao na hawana haja yakuwa katika jamii au kuendeleza maisha ya jamii. Umuhimu wa jamii na majukumu ya jamii jinsi Biblia inavyoeleza, yamekeukwa na hayapo tena sasa. Kwa sababu leo wengi wamekosa kuiheshimu jamii na kutekeleza majukumu yao kikamilifu katika nuru ya neno la Mungu, basi tunahitaji kujikumbusha na kujua vipi leo

tunapaswa kuiishi kama jamii na kuwalea watoto wetu kwa utukufu wa Mungu.

**Kwanza, kuwalea watoto katika adabu na maonyo ya Bwana ni jambo ambalo lipaswa kufanyika katika jamii na kufanywa na wazazi.**

Hili ni jambo ambalo linasisitizwa katika Biblia yote. Hili si jukumu la shule au mwalimu yeyote hata kama shule hiyo inaonekana kuwa nzuri sana katika nidhamu na iwe ni ya kikristo. Ni jukumu la wazazi kuwalea watoto wao katika adabu na maonyo ya Bwana. Hili jukumu wamepewa na Mungu na wanapaswa kulitekeleza kikamilifu na kwa utiifu. Ninasema hivi kwa sababu sisi sote tunajua kwamba siku za leo wazazi wengi wamepuza jukumu hili na wamelipeana kwa waalimu wa mashule. Kwa sababu hii wengi wanawapeleka watoto wao katika shule za kuishi huko kwa sababu wanasema, nataka mtoto wangu apate nidhamu na atoke miongoni mwa vikundi vya watu wabaya.

Tunapaswa kujua kwamba mahali ambapo mtoto anapaswa kushawishika katika maisha yake panapaswa kuwa katika jamii yake. Jamii ndio msingi wa kila nchi na watoto wanazaliwa katika jamii na kwa hivyo ni katika jamii watoto wanapaswa kuongozwa na kufundishwa. Hivi ndivyo Biblia inavyofundisha kila wakati. Maendeleo ya kiduni mara kwa mara huwa inaondoa ukweli wa Biblia na ukweli huo unapoondolewa ndivyo jamii zinapoendelea kupotea katika dhambi.

Unaposoma katika Agano la Kale utapata kwamba baba katika nyumba ndiye alikuwa kiongozi ambaye alihitajika kuongoza jamii yake katika mambo ya kujua Mungu na mapenzi yake. Yeye alikuwa na jukumu la kuwaonya watoto wake na kuwafundisha neno la Mungu. Biblia inafundisha kwamba ni jukumu la wazazi kuwalea watoto wao kila wakati kila mahali. Ikiwa tunadai kwamba sisi ni wakristo, tunapaswa kufahamu kwamba majukumu yetu kwa watoto wetu, ni jambo ambalo Mungu mwenyewe amepanga na kutuamuru tulifanye katika nyumba zetu, jamii zetu na manyumbani mwetu.

Je, wazazi wanapaswa kufanya nini haswa katika kuwalea watoto wao? Wao wanafaa kuwafundisha mafundisho neno la Mungu na kuhakikishwa wao wanaishi maisha yao katika ukweli wa neno la Mungu. Mahubiri yanafaa kufafanuliwa na kuonyesha jinsi watu wanapaswa kuishi maisha yao kulingana na mahubiri hayo. Hili ni jukumu la wazazi kuhakikisha kwamba wanaendelea kuwafundisha

watoto wao mafundisho ya kanisa na kuwasadia kuisha maisha yao kulingana na mafundisho hayo.

Swali langu kwa wazazi wote ambao wameokoka, je, wewe unawalea watot wako jinsi neno la Mungu linasema? Tunafaa kutekeleza majukumu yetu kwa sababu zifuatazo:

Kwa sababu ya yale ambayo yanafundishwa katika mashule ambamo watoto wetu wanaenda.

Shule zinafundisha kwamba wanadamu wemetoka katika wanyama. Mafundisho haya yanafundishwa kwa njia ambayo yanapaswa kuonekana ni ya kweli na ikiwa mtu hayaamini yeye anaonekana kuwa mtu ambaye haelewi chochote. Watoto wetu wanafundishwa mambo mabaya katika mashule, wanasikia mambo haya kwa redio na kuyaona kwa runinga. Mambo haya yote kusudi lake ni kuwafanya watu wasimjue Mungu, wasiamini katika Biblia na wasiwe wakristo. Je, ni nani ambaye ataweza kuwasaidia watoto wako? Ni wewe mwenyewer mzazi, biblia inakuamuru uwalee watoto wako katika adabu na maonyo ya Bwana. Wazazi wa leo, inatulazimu tufanye kazi hii kwa uangalifu sana na kwa bidii kubwa sana kwa sababu siku hizi ni mbaya sana. Wazazi ambao wameokoka wako na kazi ngumu sana ya kuwalinda watoto wao kwa sababu kile ambacho tunapigana nacho leo kina nguvu sana na kinajaribu kuwapotosha watoto wetu kila wakati.

**Pili, ninataka kuonyesha jinsi tunapaswa kuwalea watoto wetu katika adabu na maonyo ya Bwana.**

Ukweli ni kwamba kuna njia ambayo italeta madhara makubwa sana ikiwa tutaitumia katika kutekeleza majukumu yetu ya kuwalea watoto wetu katika adabu na maonyo ya Bwana. Swali ni, je tunapaswa kufanay kazi hii kwa njia gani?

Ikiwa tutawalea watoto wetu vyema katika adabu na maonyo ya Bwana, hatufai kuwaonyesha kwamba bora wametekeleza mambo fulani katika maisha yao, basi kila kitu kiko sawa. Hatufai kuwafundisha kwamba maisha ya ukristo inahusu kufuata sheria fulani Fulani na ikiwa wataishi maisha hayo ndipo basi mambo yatakuwa sawa na wao. Ikiwa tutawaonyeshe hivi, basi watapata kwamba ukristo ni jambo ambalo halina furaha yoyote na mwishowe watapendezwa na ulimwengu na kufuata ulimwengu na vitu vyake.

Tunapaswa kuwaonyesha kwamba mkristo ni mtu ambaye anapaswa kujukumika katika maisha yake yote popote Mungu amemweka. Tunapswa kuwa mfano mwema katika maisha yao na kuwafundisha

neno la Mungu wakati huo huo sisi wenyewe tukiwa tunaisha maisha yetu kulingana na neno hilo. Hatufai kuwa wanafiki wakati tunawafundisha neno la Mungu. Hatufai kuwaeleza kwamba kwa sababu wao ni watoto wanapaswa kutii ilhali sisi wenyewe hatuti. Ukristo si maisha ya kiboko au kulazimishiwa, ikiwa tutakuwa wangalifu kuishi maisha kwa utukufu wa Mungu, watoto wetu wataona na watapendezwa kufuata mfano huo huo.

**Tatu, katika majuku yetu ya kuwalea watoto katika adabu na maonyo ya Bwana, tuhakikishe kwamba hatuwalazimishi watoto wetu kufanya uamuzi Fulani.**

Kuna wengi ambao wamejiletea shida kubwa sana kwa sababu waliwalazimisha watoto wao kufanya uamuzi fulani katika maisha yao, ilhali watoto wenye hawakuwa tayari kufanya uamuzi huo. Utapata mzazi akisema, mtoto wangu alimkubali Kristo. Lakini utapata kwamba ni mzazi ambaye alimlazimisha mwanamwe kufanya uamuzi huu kwa sababu hivyo ndivyo mzazi alitaka. Ikiwa mzazi anafanya hivi, atakuwa anamyima mtoto nafasi ya kujiamulia kile ambacho anajua ni cha kweli na kinafaa. Hakuna haja ya kumwambia mtoto wako arudie ombi fulani ilia pate kuokoka. Hii siyo njia ya wokovu. Ukifanya hivi, utakuwa hata wewe mwenyewe unaonyesha kwamba hauijui njia ya kuokoka hata kidogo. Ukweli ni kwamba mtoto mdogo unaweza kumwambia chochote kama mzazi na atakikubali na atakifanya. Lakini hata hivyo, hufai kumlazimisha aokoke au katika jambo lolote.

Kila wakati tuhakikishe kwamba tunaeleza watoto wetu kwamba Kristo ndiye kiongozi wa nyumba yao na tutafanya hivi kutokana na jinsi tunavyoishi maisha yetu katika nyumba zet. Wazazi wanapaswa kuishi katika nyumba wakiwa wanaongozwa na Kristo Yesu; wao wakiwa chini ya Yesu Kristo na Kristo akiwa ndiye kichwa chao. Jambo hili lazima lionekane katika maisha yao. Wao wanapaswa kuonyesha upendo, kwa sababu upendo ni tunda la Roho Mtakatifu. Ikiwa nyumbani mwao mmejawa na upendo, basi shida zao nyingi zitaweza kutatuliwa kwa njia bora. Hivi ndivyo wazazi wanapaswa kuwalea watoto wao katika adabu na maonyo ya Bwana na si kwa kuwalazimisha kufanya uamuzi wa kuokoka au jambo lingine lolote. Si kuwaambia warudia maombi fulani fulani. Upendo wa Kristo katika nyumba ndio msingi na ushuhuda mkubwa kwa watoto wao.

# MAJUKUMU YA WAZAZI KATIKA KUWALEA WATOTO WAO

## J. C. Ryle (1816-1900)

*"Mlee mtoto katika njia impasayo, Naye hataiacha, hata atakapokuwa mzee" (Mithali 22:6).*

Mstari huu unajulikna na wengi na hata wengi wameunukuu sana katika mafundisho yao na hata kuusoma mara kwa mara. Lakini unapouangalia vizuri utaona kwamba ni wachache sana ambao wametii mafundisho ya mstari huu. Wengi wamepuuza mafundisho yake hata kama wanaujua vizuri. Huu ndio ukweli katika maisha ya wengi ambao ni wazazi.

Mafundisho ya mstari huu yamekuwepo tangu mwanzo. Lakini unapotazama sasa utaona kwamba kuna mambo mengi amabyo yametokea, Kila siku tunasikia kwamba kuna shule mpya ambazo zimeanzishwa na mafundisho mengi ambayo yametokea. Vitabu vingi ambavyo vimechapishwa na vinaeleza mambo mengi sana kuhusu kuwalea watoto. Lakini hata hivyo, watoto wengi bado hawaongozwi katika njia ambamo wanapaswa kuenenda, kwa sababu unapowaona wakati wamekuwa watu wazima, katika maisha yao hakuna kumcha Mungu na hawatembei na Mungu kamwe.

Swali ni, je kwa nini ikawa hivi? Jibu ni kwamba amri hii kutoka kwa Mungu haizingatiwi na kwa hivyo ahadi ya Mungu katika mstari huu haitimiki. Hili jambo ambalo linapaswa kutufanya wazazi kuchunguza katika mioyo yetu. Kila mmoja wetu anapaswa kujiuliza, je, ninatekeleza majukumu yangu ipasavyo? Hili ni jambo ambalo linahusu wote. Hili ni jambo ambalo linahusu kila mtu; wazazi, madaktari, walimu, mandugu, madada na wengine wengi. Katika mafundisho haya, ninataka kufundisha kuhusu jambo hili ili kila mmoja wetu apate kuelewa nini Mungu anasema na jinsi tunapaswa kutii.

**Ikiwa utamlee mtoto wake impasavyo, basi ni lazima umlee katika njia impasavyo na wala si katika njia itakayo.**

Kumbuka kwamba watoto wote wanazaliwa wakiwa wenye dhambi. Kwa hivyo ikiwa utawacha wenyewe wajichagulia jinsi wanataka, ni

wazi watachagua njia ya dhambi. Hakuna mazazi ambayo anaweza kusema kwa hakika kwamba anajua jinsi mtoto wake atakavyokuwa akiwa mkubwa. Kwa mfano hawezi akajua kama atakuwa mrefu au mfupi,m wenye nguvu au mndhaifu, mwerevu au la. Yeye anaweza kuwa chochote miongoni mwa haya yote. Lakini kile ambacho mzazi anapaswa kujua kwa kweli ni kwamba mtoto huyu ni mwenye dhambi. Ni kawaida yetu kufanya dhambi kwa sababu hivyo ndivyo tulivyo na hiyo ndiyo hali ya kila mtu ambaye hajaokoka. Biblia inasema kwamba, "Ujinga umefungwa ndani ya moyo wa mtoto" (Mithali 22:15), "...mwana aliyeachiliwa humwaibisha mamaye" (Mithali 29:15). Mioyo yetu ni kama ardhi, ikiwa haishughulikiwa, italeta magugu.

Kwa hivyo ikiwa utamsaidia sana mtoto wako, basi hufai kumwachilia ajiongoze. Msaidie kama tu vile ungemsaidia mtu ambaye ni kipovu. Usimwachilie afanye jinsi anavyotaka kwa sababu atajipoteza. Wewe hufai kufuata mapenzi yake, na kumwachilia afanye jinsi anavyotaka, unapaswa kumwongoza kikamilifu. Yeye bado hajajua nini ambacho ni kizuri kwa nafsi yake na akili ya mtoto wako. Kwa kawaida si watoto ambao huwa wanaamua watakula nini au watava nini. Ni lazima tuwe wakakamavu katika kuwawalea watoto wetu. Tuwalee watoto wetu kulingana na mafundisho ya Biblia na si katika njia ambayo wanaipenda wenyewe. Kila mtoto huwa anajaribiwa kutaka kufanya jinsi anavyotaka na ni lazima kila mzazi ahakikishe kwamba anafanya jukumu lake la kumlea mtoto wake kulingana na mafundisho ya Biblia na wala si kulingana na jinsi mtoto mwenyewe anataka.

Pia mlee mtoto wako kwa upendo na uvumilivu. Simaanishi hapa kwamba uharibu maisha ya mtoto wako. Upendo ndilo jambo ambalo linafaa kutuongoza katika majukumu yetu yote juu ya watoto wetu. Tunfaa kuwa wazuri, wakarimu, wavumilivu, wenye utu wema na kupenda kujua shida za mtoto. Ni lazima tuwe tayari kufurahia na watoto wetu wakati wa furaha, hii itatusaidia sana kuwalea na kuwaogoza watoto wako. Haya ni mambo ambayo tunapaswa kuyashughilikia ikiwa kweli tutaweza kuwasaidia watoto watu kuenenda katika njia ya Mungu.

Hata kama mtoto ni wako, jua kwamba hata yeye ako na moyo na anaweza kushushua moyo kama tu wewe. Ikiwa mzazi ni mtu mgumu na kila wakati yeye ni mtu ambaye hana wakati wa kuongea au kujua nini inaendelea katika maisha ya mtoto wake, yeye atamfanya mtoto wake ashushwe moyo sana katika maisha yake. Tabia hii itamfanya mtoto akose kukueleza lolote katika maisha yake na hii itakuwa vigumu sana wakati unataka kuzungumza naye. Lakini ikiwa watoto wako

wataona kwamba kweli wewe ni mtu ambaye anawapenda na kwamba unawatakia mazuri katika kuwalea kwako, na kwamba hata wakati unawaadhibu ni kwa uzuri wao na kwamba hata uko tayari kufanya lolote kwa ajili ya maisha yao, utaona kwamba wao watakupenda na litakuwa jambo rahisi sana kwako kuwaongoza katika neno la Mungu. Kumbuka kwamba lazima uwe mtu mwenye upendo ikiwa kweli watafungua mioyo yao kwako. Upendo ndio jambo ambalo litakusaidia sana katika kuwalea watoto wako. Hasira na kelele ni mambo ambayo yatamtisha mtoto sana, lakini hatamshawishika katika tabia na maisha matakatifu. Ikiwa ataona kwamba kila wakati wewe ni mtu ambaye unakasirika, atakosa kukuheshimu. Baba ambaye anazungumzia mtoto wake kama Sauli alivyofanya kwa Yonathani (1 Samweli 20:30), asitarajie kuwa na ushawishi wowote juu ya mtoto huyo.

Kila mzazi anafaa kujitahidi kwamba hapotezi upendo wa mtoto wake. Ni jambo baya sana kumfanya mtoto wako akuogope, hiyo sio heshima kwako bali uoga wa kuumizwa. Uoga huwa unaondoa uwazi wa mazungumzo katika maisha ya mtoto wako. Mtoto atasema lolote bora asiumizwa na wewe mzazi. Uoga utamfanya awe mnafiki na mdanganyifu. Kwa sababu hii Biblia inasema, “Ninyi akina baba, msiwachokoze watoto wenu, wasije wakakata tamaa” (Wakolosai 3:21). Kina baba tusipuuze mstari huu ikiwa kweli tunataka kuwalea watoto wetu kwa njia ambayo ni ya kuwasaidia katika maisha yao.

**Kumbuka kila wakati kwamba katika kazi yako ya kuwalea watoto wako, nafsi yao ndio inafaa kuwa jambo la kwanza na la muhimu Zaidi.**

Ni ukweli kwamba watoto wetu ni wa muhimu sana kwetu. Lakini ikiwa kweli tuunawapenda watoto watu, kila wakati waza juu ya nafsi zao. Maisha yao ya milele linafaa kuwa jambo ambalot unalizingatia sana kuliko mambo mengine. Unafaa kukumbuka kwamba nafsi zao hazitawahi kufa na kwa hivyo lazima uwaongoze katika njia ambayo itafanya nafsi zao ziishi katika furaha ya milele. Kila kitu ambacho tunakiona leo, kitaisha. Ulimwengu na mali yake utaisha na mali pia itaisha. Lakini nafsi ambayo inayoishi katika watoto wetu ni ya milele na kwa hivyo kila mzazi lazima ahakikishe kwamba anamsaidia mtoto wake kufanya uamuzi bora ili nafsi yake isiangamie milele jahanumu. Ikiwa mtoto wako ataenda jahanum, makosa ni yako, kwa sababu umekata kumfundisha neno la Mungu na jinsi anapaswa kuishi katika ukweli wa neno hilo. Wewe unajitahidi kumpa vitu vya dunia hii ambavyo si vya milele hatakama baadhi yavyo ni vizuri kwa maisha ya

hapa duniani. Maisha ya mtoto wako ya baadaye, yaani maisha yake ya milele, yanategemea jinsi unavyomlea leo.

Hili ndilo linafaa kuwa kusudi lako kila siku katika uleze wa watoto wako. Katika kila jambo ambalo unawafanyia watoto wako, unafaa kujiuliza, je, hili ambalo ninalifanya litawasaidia aje kuingia ufalme wa mbinguni? Ikiwa utampa mtoto wako chochote anachokitaka katika maisha haya ili awe mtu wa maana, ni kukosa upendo halisi kwa mtoto wako. Kwa sababu ni kweli kwamba vitu hivyo vyote ambavyo unampa, si vya milele anapotoka katika ulimwengu, vitu hivyo havitamsaidia hata kidogo. Upendo wa kweli kwa mtoto wako ni upendo ambao unashughulikia nafsi yake kwa vyovyote vile. Usimfanye mtoto wako kuwa kama mnyama ambaye hana lolote la kutazamia katika maisha mengine. Ikiwa mtoto wako humwongoza katika neno la Mungu, ni kumficha kile ambacho ni cha muhimu sana ambacho anastahili kupewa tangu akiwa mtoto mdogo sana. Katika Biblia tunasoma kumhusu Timotheo ambaye Paulo alimwandikia akimwambia kwamba, "...na ya kuwa tangu utoto umeyajua maandiko matakatifu, ambayo yanaweza kukuhekimisha hata upate wokovu.." (2 Timotheo 3:15). Mtoto wako anastahili kuokoka, kwa sababu hili ndilo kusudi la Mungu katika maisha yake.

Mkristo hafai kuwa mtu ambaye anafuatana na mitindo ya ulimwengu na kumfanya mtoto wake kubishana na walimwengu katika mitindo yao badala ya kufunza mtoto wake njia ya mbinguni. Hatufai kufanya mambo kwa sababu hivi ndivyo ulimwengu unavyofanya. Hatufai kuwalea watoto wetu katika njia za dunia kwa sababu hivyo ndivyo ulimwengu unavyofanya na kutaka. Kwa mfano, ulimwengu unajizatiti sana kuona kwamba watoto wake wanakuwa na elimu ya juu ili waweze kuishi maisha mazuri. Si vibaya hata kwa wakristo kuelimisha watoto wao hata katika vyeo vikuu, lakini ikiwa tutazingatia tu hili la masoma makubwa na kusahau nafsi ya mtoto basi tutakuwa tumekosa sana mbele za Mungu. Jambo la kwanza ambalo tunahitaji kuzingatia sana ni kwamba, watoto wetu wanamjua Kristo. Hatufai kuwaacha watoto wetu wasome vitabu fulani kwa sababu vinasomwa na wote na kuona mambo fulani katika runinga kwa sababu yanaonwa na wote; au kusikia miziki fulani kwa sababu inasikilizwa na wote. Hatufai kuogopa kuitwa wajinga au wasioelimika kwa sababu ya jinsi tunayowalea watoto wetu katika njia ya Bwana. Mzazi ambaye amemlea mtoto wake kwa ajili ya mbinguni na wala si kwa ajili ya ulimwengu, huyu ndiye anaitwa mzazi mwenye hekima.

**Katika kumlea mtoto wako, mfundishe mtoto wako kujua neno la Mungu.**

Ni kweli kwamba hakuna mzazi ambaye anaweza kumfanya mtoto wake alipende neno la Mungu. Hii ni kazi ya Roho Mtakatifu pekee yake. Ni Yeye ambaye anatupatia tamaa ya neno la Mungu. Lakini hata hivyo unaweza kuwafanya watoto wake waijue Biblia.

Kuwa na kufahamu kuzuri juu ya Biblia ndio msingi wa kuwa na matazamo wa kweli wa dini ya ukristo. Wale ambao wameijua Biblia, si rahisi watu hao kuyumbishwa-yumbishwa na kila aina ya mafundisho ya uongo. Aina ya kufundisha ambayo haizingatii kufahamu Biblia vyema, haifaa kukubalika popote kwa sababu huo ndio msingi wa mafundisho ya uongo.

Tunafaa kuwa waangalifu katika hili jambo kwa sababu katika makanisa kuna wale ambao wanahubiri ukweli kwa Kristo kwamba ndiye mwokozi na kuna wale ambao wanahubiri kwamba mambo kama meza ya Bwana ndio msingi wa kuingia mbinguni. Pia kuna wale ambao wanazingatia sana vitabu fulani za dini kuliko Biblia na katika kulea kwao kila wakati wanaeleza tu watoto wao hadithi na hawawasomei Biblia. Ikiwa unapenda watoto wako, wafundishe Biblia pekee yake. Usitaka kuwafanya wajue yale yaliyomo katika vitabu vingine, badala yake wacha waijue Biblia. Huku ndiko kulea na kufundisha ambako Mungu aneheshimu na ambako kunaleta wokovu katika nafsi ya mtoto. Biblia inasema, "...kwa maana umeikuza ahadi yako, kuliko jina lako lote" (Zaburi 138:2). Mungu huwa anawabariki wote ambao wanaliheshimu neno lake miongoni mwa wanadamu wote.

Pia hakikisha kwamba watoto wako wanasoma Biblia wakifahamu mwamba ni neno la Mungu. Wakumbushe kwamba Biblia si neno la mwanadamu bali ni neno la kweli la Mungu. Waeleze neno la Mungu ni la kweli na linafaidi na liko na nguvu za kuleta wokovu kupitia kwa imani ndani ya Yesu Kristo.

Hakikisha kwamba watoto wako wanasoma neno la Mungu kila siku. Wafundishe kujua kwamba neno la Mungu ni chakula cha kila siku cha nafsi zao. Hi sasa haimaanishi kwamba wanapaswa kuona hii kama jukumu tu, kwa sababu jinsi wanavyoendelea kusoma Biblia indivyo watakapoendelea kujua Mungu na Roho Mtakatifu ndivyo atalavyoedelea kuwazungumzia kila siku kupitia kwa neno la Mungu.

Hakikisha kwamba wanalisoma kwa pamoja. Usiogope kuwafundisha mafundisho ya msingi katika Biblia. Usiwaze kwamba wao

hawataelewa hata kidogo. Huu siyo ukweli kwa sababu watoto wadogo wako na uwezo wa kufahamu mambo kuliko hata sisi watu wazima.

Hakikisha kwamba unawafundisha kuhusu dhambi, hatia ya dhambi, madhara ya dhambi, nguvu za dhambi, na uovu wa dhambi.

Hakikisha kwamba unawafundisha kuhusu Yesu Kristo na kazi ambayo alifanya msalabani kwa ajili ya wokovu wetu. Lazima tuwafundishe kuhusu kifo cha Yesu Kristo, msalaba wa Kristo, sadaka ya Kristo, damu ya Kristo na kazi ya Kristo akiwa Kuhani Mkuu.

Hakikisha unawafundisha kazi ya Roho Mtakatifu katika mioyo ya wanadamu. Jinsi Roho Mtakatifu anavyowabadilishwa wanadamu na kuwazaa mara ya pili. Kazi ya Roho Mtakatifu kuwafanya wawe watakatifu. Pole pole utaona kwamba watoto wako wanaanza kuelewa. Tusije tukawaza kwamba wao hawawezi kujua au kufahamu lolote katika Biblia.

Hakikisha kwamba anawafundisha watoto wako neno la Mungu kila wakati. Wacha maisha yao yawe yamejazwa na neno la Mungu. Wacha neno la Mungu likae ndani mwao. Hakikisha kwamba unawanunulia Biblia na unawahimiza wasome Biblia hiyo kila wakati. Soma na wao, omba na wao na pia wahimiza kusoma pekee yao na waombe. Wahimize kila wakati kumwomba Mungu msamaha wa dhambi zao hadi siku ile watakuwa na uhakika katika mioyo yao kwamba wameokoka.

**Pia hakikisha kwamba unawafundisha kuomba.**

Maombi ni ishara kwamba mtu anaishi kiroho. Hii ndio ishara ya kwanza kwamba mtu kweli amezaliwa mara ya pili. “Bwana akamwambia, simama, enenda zako katika njia iitwayo Nyofu, ukaulize katika nyumba ya Yuda mtu aitwwaye Sauli, wa Tarso; maana, angalia, anaomba” (Matendo ya Mitume 9:11). Sauli alikuwa ameanza kuomba na hiyo ilikuwa ishara tosha kwamba alikuwa amebadilika. Maombi ndio ilikuwa ishara kati ya watu wa Mungu na wale ambao si Mungu; wanadamu walianza kuliita jina la Bwana (Mwanzo 4:26). Wakristo wote leo ni watu wa maombi. Wanaomba kwa sababu wanamwambia Mungu mahitaji yao, hisia zao, tamaa zao, uoga wao. Wakati wanaomba wao huwa wanamaanisha kile ambacho wanasema kwa Mungu. Yule ambaye hajaokoka, yeye anaweza kurudia maombi fulani na hata yawe mazuri, lakini ukweli ni kwamba yeye haombi hata kidogo.

Maombi ni jambo ambalo linaazisha mabadiliko katika nafsi ya mwanadamu. Kazi ambazo tunafanya za hudumu haziwezi kufaulu bila maombi.

Maombi ni chombo ambacho kinaleta ufanisi katika mambo ya kiroho. Ikiwa mtu anamaliza muda katika maombi, atapata kwamba mtu huyu atakua kiroho. Kwa hivyo ikiwa hatutajitahidi katika maombi, hatutakuwa jinsi tunapaswa kukua. Mkristo amabye anaendelea vyema kiroho ni yule ambaye anasoma neno la Mungu kila siku na analitii na pia ni yule anajitahidi katika maombi. Yeye huwa anaomba mengi na anapata mengi. Yeye kila wakati huwa anamwambia Yesu kila kitu na huwa anajua jinsi ya kutenda katika hali zote.

Maombi ndio chombo ambacho Mungu ameweka katika mikono yetu. Ndio silaha bora ya kutumia katika kila hali. Ndicho kifungua ambacho kinafungulia ahadi na baraka za Mungu na ndio mkono wa neema wakati wa mahitaji. Maombi ndio sauti ambayo Mungu anasema tupaze katika kila jambo, katika kila hali na ndio kilio ambacho Mungu ameahidi kusikiliza kila wakati.

Maombi ndio njia rahisi mwanadamu anapaswa kutumia kuja kwa Mungu. Kila mtu anaweza kuomba; mgonjwa, mzee, kiwete, kipovu, maskini, mwenye hajasoma, tajiri; wote wanaweza wakaomba. Kwa hivyo hakuna mtu ambaye anaweza kusema kwamba hana uwezo wa Kuomba. Maneno ya Yakobo yatahumu wengi siku ya hukumu. Yakobo aliandika akisema, “Mwatamani, wala hamna kitu, mwaua na kuona wivu, wala hamwezi kupata. Mwafanya vita na kupigana, wala hamna kitu kwa kuwa hamwombi” (Yakobo 4:2).

Ikiwa unawapenda watoto wako, basi hakikisha kwamba unawafundisha tabia ya kuomba. Wafundishe jinsi wanapaswa kuomba. Wakumbushe kwamba ikiwa hawataomba, hawatapata chochote kutoka kwa Mungu.

Hii ndiyo hatua ya kwanza katika dini ambayo mtoto yeyote anaweza kufuata. Kabla hajajua kusoma, mfundishe kuomba. Hatua ya kwanza ya mtoto katika maisha yake ni ya muhimu sana, vivyo hivyo, hatua ya kwanza katika maisha ya ukristo ya mtoto ni ya muhimu sana. Jinsi wanavyoomba ni jambo la muhimu sana na kwa hivyo tunapaswa kulizingatia sana. Ni lazima tuhakikishe kwamba tunawaonyesha jinsi ya kuomba ili wasiwe watu wakusema tu maneno matupu kwa haraka sana. Hili ndilo jambo ambalo tunaweza kusikia na kuona likifanywa na watoto wetu. Ikiwa hujawahi kusikia mtoto wako akiomba, basi ni wewe wa kulaumiwa.

Maombi ndilo jambo ambalo tunaweza kukumbuka sana hata baada ya muda mrefu.

Unaweza ukatutana na mtu ambgaye ni mzee na akuelezee jinsi alivyofundishwa kuomba na mzazi wake. Mambo mengi yanaweza kuwa yamesaulika naye, lakini si rahisi kusahau jinsi alivyofundishwa kuomba na mzazi wake. Anaweza kusahau marafiki wake wa zamani au mchungaji wake, lakini huenda asisahau maombi yake ya kwanza.

Msomaji, ikiwa unawapenda watoto wako, wafundishe kuomba. Ikiwa unawafundisha katika mambo mengine, hakikisha kwamba wanajua kuomba.

# Kuwafundisha watoto kumhusu Mungu

## Philip Doddridge (1702-1751)

Kazi ya kumwokoa mwadanamu ni kazi ya Mungu pekee. Si mahubiria ya mhubiri ambayo yanamwokoa wenye dhambi wala si nguvu za mtu yeyote, bali ni kazi ya Roho mtakatifu katika moyo wa mwanadamu ambapo mtu anapata kuokolewa. Lakini hii haimaanishi kwamba kama wazazi tunafaa kupuuza majukumu yetu ya kuwafundisha watoto wetu neno la Mungu. Mungu ameweka mipangilio fulani katika ulimwengu ambayo anaitumia kutekeleza mapenzi yake. Ni ukweli kwamba Mungu hamwongoji mwanadamu yeyote ili afanye mapenzi yake, lakini hata hivyo mtu yeyote asitarajie kwamba Mungu ataacha kutumia njia ambazo ameweka kutekeleza mapenzi yake. Kwa mfano Mungu amesema ndipo wanadamu wapata kuokoka, lazima alisikia neno lake na aliitii (Warumi 10:14-17). Kwa hivyo ikiwa mchungaji fulani hatahubiri neno la Mungu kwa uaminifu, ni wazi kwamba hakuna mtu amabye ataokoka miongoni mwa wale ambao anahubiria. Lakini Mungu anaweza kumtumia mtu mwingine kunena neno lake katika maisha ya mtu, na mtu huyu apate kuokoka. Njia ya wokovu ni kusikia na kutii neno la Mungu, bila kusikia na kutii, kamwe hakuna wokovu kwa mtu yeyote.

Biblia inasema kwamba, “Mtu haishi kwa mkate tu, ila kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu” (Mathayo 4:4). Mstari huu haumaanihi kwamba sasa hatufai kufanya kazi ya kuwalinda na kuwapa

chakula watoto wetu, ikiwa tutafanya hivyo, na watoto wetu wafe kwa sababu ya njaa, tutakuwa na hatia machoni pa Mungu ya kuwaua watoto wetu. Vivyo hivyo, tusije tukajidanganya kwamba watoto wetu wanaweza kumjua Mungu bila sisi kujukumika kwa kuwafundisha neno lake kila wakati. Mungu ametupatia jukumu kubwa sana na tunafaa kuhakikisha kwamba watoto wetu wanaokoka. Hili ni jukumu ambalo kila mzazi anapaswa kutii.

**Tunafaa kuwafundisha watoto wetu kumcha na kujitolea kwa Mungu.**

Huu ndio msingi wa kila kitu ambacho ni kizuri: “Kumcha Bwana ndio mwanzo wa hekima” (Zaburi 111:10). Kwa sababu hii mwandishi wa Zaburi anawaita watoto wote ili waweze kufundishwa kumcha Bwana: “Njoni enyi wana, mnisikilize, Nami nitawafundisha kumcha Bwana” (Zaburi 34:11). Ni lazima kwanza tuwafundishe watoto wetu kuhusu Mungu kabla ya kuwafundisha misingi ya mafundisho ya Biblia ambayo yanamhusu Kristo akiwa mwakilisha wetu mbele za Mungu. Biblia inafundisha kwamba, pasipo Imani haiwezekani kumpendeza; “kwa maana mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba Yeye yuko, na kwamba huwapa thawabu wale wamfuatao” (Waebrania 11:6).

Ukweli kumhusu Mungu na jinsi alivyo ni mambao ambayo kwanza lazima mtoto wako ayafahamu. Mtoto wako afahamu kwamba mjenzi wa kila nyumba ni mwanadamu, na kwa hivyo lazima pia afahamu kwamba Mungu ndiye mjezi wa kila kitu. Kutokana na jambo hili kwamba Mungu ndiye muumba wa kila kitu, na kwamba Yeye ni Mkuu na ni Mwema, basi watoto wetu lazima wafahamu kwamba wanastahili kumcha Mungu na kumletea utukufu wote.

Ni jambo la muhimu sana kwamba watoto wanamcha Mungu na kunyenyekea katika utakatifu na utukufu wake. Kwa hivyo tunapaswa kuwaeleza kwamba Mungu ni mkuu kuliko watu na vitu vyote. Wakati tunataja viumbe vingine kama malaika, wanadamu na shetani, ni lazima tuwaelezea kwamba viumbe hivi viko chini ya utawala wa Mungu. Kwa hivyo wanapotaja jina la Mungu, hawapaswi kulitaja kwa mzaa au bure. Bali wanapaswa kujua kwamba Mungu ni Mungu na wao na sisi wazazi wao ni mavumbi tu. Ikiwa utawafundisha watoto wako hivi, basi utakuwa umetekeleza majumu yako kwa utukufu wa Mungu. Watakuwa wakimcha Mungu, kwa sababu Yeye ni Mungu.

Wakati pia tunawafundisha kumhusu Mungu tuhakikishe kwamba hatuwaogopeshi na kuwafanya wamwogope kwa njia ambayo hata wakataa kumkaribia. Tuwafundishe kwamba Mungu ni Mkuu lakini

pia Mungu ni mwema. Tuwafundishe kumfahamu kama: “BWANA, BWANA, Mungu mwingi wa huruma, mwenye kuwaonea huruma, mwenye fadhili, si mwepesi wa hasira, mwingi wa rehema na kweli; mwenye kuwaonea huruma watu elefu, elefu, mwenye kusamehe uovu na makossa na dhambi; wala si mwenye kumhesabia mtu mwovu kuwa hana hatia kamwe; mwenye kuwapatiliza watoto uovu wa baba zao, na wana wa wana wao pia, hata kizazi cha tatu na cha nne” (Kutoka 34:6-7). Tunafaa kuwafundisha kwamba Mungu ako kila mahali na kwamba anavipenda viumbe vyake na kwamba Yeye huvipa viumbe vyake kila kitu vifurahia. Tunafaa kuwakumbusha kwamba wao wanaishi kwa sababu Mungu amewafanya waishi. Na kwamba pia wanafaa kupenda Mungu ambaye ametupatia uwezo wa kuwapenda na kuwasaidia katika maisha yo.

Pia tunapaswa kuwakumbusha kwamba wao siku moja watakufa na kusimama mbele za Mungu. Na kwamba Yeye sasa yuko nao na anajua kila kitu ambacho wanakifanya, wanawaza na kuongea na kwamba siku moja atawaleta katika furaha ya milele au katika taabu ya milele ikiwa watakuwa wametii neno lake au wamelikataa. Kwa hivyo tunapaswa kuwaeleza kwa wazi kabisa kuhusu jahanum na mbinguni kulingana na mafundisho ya Biblia.

Ikiwa msingi mwema kumhusu Mungu utawekwa katika maisha ya watoto wetu na hali ya maisha yao ya badaye ya mbinguni au jahanum, basi ni wazi kabisa kwamba ni lazima tuwaeleze majuku yao kwa Mungu. Haswa haswa wanapaswa kufundishwa jinsi ya kumwomba Mungu na kumleta sifa. Ni vizuri kuwafundisha kumwomba Mungu kutoka katika mioyo yao na wala si tu kurudia maneno fulani ambayo utawambia. Lakini kabla wenyewe wafikie kuomba kutoka katika mioyo ya, ni wazi kwamba lazima tuwasadia na kuwafundisha jinsi wanapaswa kuomba kulingana na Biblia.

## Pili, tunafaa kuwafundisha watoto katika njia ya Imani ndani ya Kristo Yesu.

Biblia inatukumbusha kwamba, Yesu Kristo, ndiye, njia, ukweli na uzima (Yohana 14:6). Ni kupitia kwake Kristo tunapa ujasiri wa kuja mbele za Mungu ambaye Biblia inamwita “moto ulao.” Kwa hivyo ni jambo la muhimu sana kuwaongoza watoto wetu katika kumfahamu Yesu Christ kwa sababu hivyo ndivyo inavyomaanisha kuwalea watoto katika adabu na maonyo ya Bwana (Waefeso 6:4).

Tunafaa kuwafundisha kwamba wazazi wetu wa kwanza, yaani Adamu na hawa, walimwasi Mungu na wakaanguka katika dhambi pamoja na watoto wao ambao ni sisi. Kwa sababu ya dhambi yao, laana ya Mungu ilikuja katika ulimwengu huu (Mwanzo 1-3). Tunafaa kuendelea kuwaonyesha madhara ya dhmabi hii katika ulimwengu na katika maisha yao. Lakini pia tukumbuke kuwaeleza kwa wazi kwamba wao hawawezi kusingizia Adamu na Hawa kwa sababu ya uovu wao. Wao kama wanadamu pia wamemkosea Mungu na Mungu amekasiri na wao. Kwa hivyo wao wako na hatia mbele za Mungu na wanapaswa kuhakikisha kwamba hati hiyo inaondolewa kwao na Mungu. Tunapaswa kuendelea kuwafundisha kufundisha njia ya wokovu katika imani ndani ya Kristo Yesu.

Tunapoendela kuwafundisha, tuhakikisha kwamba hatuwaonyeshi kwamba Mungu Baba ni mbaya na kwamba Kristo ni mzuri. Yaani tusije tukawafanya wawaze kwamba kuna tofauti ya Mungu Baba na Mungu mwana katika maisha yao. Tunafaa kuwaonyesha kwamba Baba ndiye mwanzilishi wa njia ya wokovu. Ni yeye ambaye ametuhurumia na kumtuma Yesu Kristo aje atuokoe kutoka katika dhambi zetu. Tunawaonyesha hivi kwa sababu hivi ndivyo Biblia inavyofundisha. Kila wakati tunapaswa kuwaeleza kuhusu utakatifu wa Mungu na huruma wa Mungu. Yeye angetaka angemwangamiza mwanadamu, lakini alimfanya mwanawe Yesus Kristo awe sadaka ya dhambi kwa ajili ya mwanadamu. Yeye alimfanya akufe ili sisi wanadamu tuishi.

Tunafaa kuwaeleza kwamba Kristo Yesu hakulazimishwa kufa kwa ajili ya dhambi zetu. Yeye alijitolea afe ili sisi tupate kuokolewa. Biblia inasema, “Tazama, nimekuja (katika ngombo la chuo nimeandikiwa) Niyafanye mapenzi yako, Mungu” (Waebrania 10:7,9). Tunafaa kuwafundisha Kristo Yesu ni nani. Yeye ni Mungu aishiye milele, Yeye ni mkuu kuliko malaika na wanadamu. Tunafaa kuwafundisha kuhusu yale ambayo Kristo aliyapitia ili aweze kutuokoa. Yeye alifanyika mwanadamu, alikataliwa, aliteswa na alikuwa mtu wa huzuni na aliuliwa msalabani, yote kwa ajili ya dhambi zetu. Tunapaswa kuwaeleze kwamba wanafaa kuwa na shukrani kwa Kristo kwa sababu yale ambayo ametufanyia sisi wenye dhambi. Tuwafundishe kuhusu upendo wa Kristo kwa watu wote hata watoto kama wao. Aliwakemea Wanafunzi wake wakati walijaribu kuwakataza watoto wasije kwake: ‘Wacheeni watot wadogo waje kwangu, wala msiwazuie, kwa kuwa watu kama hao ufalme wa Mungu ni wao” (Luka 18:16). Haya yaliandikiwa ili watoto waone na wajue kwamb Kristo anajali hata watoto.

Tuwaonyesha kuhusu kifo cha Kristo. Kwamba Kristo alijitoa mwenyewe na hakulazimishwa na mtu yeyote. Alionyesha hili katika maneno yake kwa wale ambao walikuwa wamekuja kumshika katika bustani ya Gethsemane (Yohana 18:6). Yeye alipigwa sana, alitemewa mate na alivalishawa taji la miiba na kubebeshwa msalaba ambao alisulubiwa juu yake. Tunafaa kuwafundisha kwamba Kristo alitenda haya yote, lakini hakuwa na dhambi yoyote. Wakati walipomsulubishwa, Yeye badala ya kuwalaani, Yeye aliwaombea kwa Mungu (Luka 23:34). Tuwaeleze kwamba haya yote yalimfanyika Kristo kwa ajili ya dhambi za sisi sote.

Pia tuwafundishe kuhusu kufufuka kwa Kristo na kurudi kwake mbinguni. Na kwamba sasa ako mbinguni akiendelea kuwaombea watu wake ambao wamemwamini na wale ambao watamwamini.

Tuendelea sasa kuwafundisha juu ya kutii Mungu katika mambo haya yote, Wakati huo huo kuwakumbusha wao kuhusu udhaifu wao na dhambi zao hata baada ya kuokoka. Na kwamba Mungu huwa anamtuma Roho Mtakatifu katika mioyo ya wale ambao wameokoka ili awasaidie kufanya mapenzi ya Yake, yaani kazi njema ambazo zinamletea Mungu utukufu. Haya ni mambo ya muhimu sana kuwafundisha watoto wetu, na ikiwa hatutawalea katika kumcha Mungu, basi chochote tunafanya kitakuwa ni kazi bure.

# NIDHAMU AMBAYO LENGO LAKE SI KUWAUMIZA WATOTO

## David Martyn Lloyd-Jones (1899-1981)

*"Nanyi akina baba, msiwachokozi watoto wenu; bali waleeni katika adabu na maonyo ya Bwana" (Waefeso 6:4).*

Katika mstari wa 1, Paulo alinukuu naneno ya sharia ambayo ni "Mheshimu baba yako na mama yake." Katika mstari wa 4, Paulo anataja "akina baba" peke yao. Kuonyesha kwamba jukumu ambalo analitaja hapa ni jukumu la akina baba. Hii ni kwa sababu akina baba ndio kichwa cha nyumba na ndio wamepewa mamlaka na Mungu kuongoza nyumba zao. Hivi ndivyo Agano la Kale lilifundisha na hivi ndivyo Mungu amekuwa akiwafundisha watu wake waishi maisha yao

katika nyumba zao. Ni jambo la kuhuzunisha kwamba, leo tunaishi katika nyakati ambamo waume katika manyumba wameachia jukumu hili akina mama. Pia hili ni jambo ambalo linamhusu yeyote ambaye anafundisha nidhamu. Katika mstari huu, tunafundishwa kuhusu jambo moja la nidhamu.

Lazima tuwe waangalifu katika jambo hili. Hili ni jambo ambalo linafaa kuzingatiwa sana kwa sababu katika kila jamii, kuna shida katika kufundisho ya nidhamu. Shida hii iko kila mahali; katika mashule, katika manyumba, mahali pa kazi na katika makanisa. Hii ndio shida kubwa sana leo ambayo tunakumbana nayo katika kila hali. Nidhamu ndio msingi wa wengi kutekeleza majukumu yao na ndio msingi wa uhusiano wowote na maandeleo mahali popote. Ikiwa tutaendela katika anasa na kuwa wazembe katika majukumu yetu ilhali tunaendelea kutaka pesa nyingi, na kuendelea katikk anasa za ulimwengu, basi ni wazi kwamba tutakuwa tumekosa nidhamu katika maisha yetu. Kuna mataifa mengi ambayo yamejipata katika shida nyingi sana za kiuchumi au kimeendeleo kwa sababu ya ukosefu wa nidhamu miongoni mwa watu wake. Hata leo tunaona jambo kama hilo katika nchi zetu. Wengi ni wanyonge sana katika kazi zao, wengi hawana nidhamu katika manyumbani mwao na hata katika jamii zao, lakini wanataka Zaidi na Zaidi. Watu wengi wanapenda kumazliza muda wao mwingi katika mambo ambayo haiwaletei faida kamwe. Kwa mfano wengi wanamaliza muda wao mwingi katika kunywa pombe au kutumia madawa au kukaa tu na kutazama michezo na vipindi katika runinga zao. Wao wanakosa kujukumika katika majukumu yao ya kila siku. Hawa wote wamekosa nidhamu katika maisha yao.

Haya ni baadhi ya mambo ambayo mwandishi wa mstari huu anatuonyesha kama matunda ya ukosefu wa nidhamu. Nitaendelea kuonyesha jinsi Biblia inavyofundisha kuhusu haya mambo yote lakini kabla sijafanya hivyo, wacha nitaja jambo ambalo litatusaidia kuwaza vizuri juu ya jambo hili la nidhamu.

Shida kubwa sana ambayo tuko nayo leo ni kwamba sisi wenyewe hatujiwazia. Unapowaangalia wengi leo, utaona kwamba wengi hawachukui muda wao mwingi kuwaza juu ya maisha yao na majukumu yao. Leo utapata kwamba magazeti, vipindi vya redio au kwa runinga ndivyo vinashawishi wengi katika mawazo yao. Hii ndio sababu wengi hupenda kufuatilia vipindi hivi kwa bidi sana. Hii ni ishara moja ya kutuonyesha kwamba wengi hawana nidhamu katika maisha yao. Ni lazima tuwe na nidhamu katika mawazo yetu. Biblia inasema, “Yeye asiyetumia fimbo yake, humchukia mwanawe” (Mithali

13:24). Pia inasema, "Nanyi akina baba, msiwachokoze watoto wenu" (Waefeso 6:4). Shida yote ya nidhamu iko katika haya mambo mawili. Ni lazima kila wakati tuhakikishe kwamba Biblia inatuongoza katika kila jambo ambalo tunakumbana nalo. Shida zetu kuhusu nidhamu zinatokana na kuegemia andiko moja kati ya Mithali 13:24 na Waefeso 6:4. Si makossa ya Biblia kwamba wengi wanaegemea upande mmoja au mwingine, makossa ni yetu kwa sababu tumekosa kuelewa na kutekeleza jinsi maandiko yanafundisha. Tuombe hekima kwamba maandiko haya yanatekelezwa kwa neema ya Mungu katika jamii zetu.

Je, tunapaswa kutekeleza nidhamu hii kwa njia gani? Kwanza kabisa, nidhamu ni ya muhimu sana na inapaswa kutekelezwa bila kuzembea. Lakini pia tunapaswa kuwa waangalifu sana jinsi tunavyoitekeleza kwa sababu isipotekelezwa vyema, inaweza kuleta madhara makubwa sana.

Mstari wa Waefeso 6:4, uko na mambo mawili ya kutufundisha. Kwanza, akina baba wanaambiwa, "msiwachokoze watoto wenu." Pili unasema, "bali waleeni katika adabu na maonyo ya Bwana." Tunapaswa kukumbuka mambo haya mawili yote ikiwa tutatekeleza jambo hili kwa uaminifu.

**Kwanza Biblia inasema, "msiwachokoze watoto wenu."**

Kwa ufupi unasema kwamba msiwafanya watoto wenu wawachukie. Hii ndio hatari ambayo tunaweza kujipata ndani wakati tunatekeleza nidhamu. Ikiwa tutakuwa na hatia katika kuitekeleza nidhamu, basi hatutawasaidia watoto wetu hata kidogo. Kama tu vile tumeona, kuegeme kifungu kimoja ni makossa makubwa sana. Kwa ufupi ni kwamba tunafaa kutekeleza nidhamu hii kwa njia ambayo hatuwafanyi watoto wetu watuchukie au wamchukie Mungu. Ni lazima tujichunge sana katika hili.

Je, tutafanya aje? Je, tutawezaje kutekeleza nidhamu ambayo haitawafanya watoto wetu watuchukie au wamchukia Mungu? Tutazama Waefeso 5:18, "Tena msilewe kwa mvinyo, ambamo mna ufisadi; bali mjazwe Roho." Maisha ya mtu ambaye anaongozwa na Roho, ni maisha ambayo yanaonekana katika mambo mawili: nguvu za Roho Mtakatifu na kuwa mtu mwenye kiasi. Nguvu za Roho Mtakatifu zinatuongoza katika nidhamu mzuri. Paulo anamwandikia Timotheo akisema, "Maana Mungu hakutupa roho wa uoga, bali ya nguvu ya upendo na ya moyo wa kiasi" (2 Timotheo 1:7). Hizi nguvu ambazo zinathibitiwa na upendo na hekima. Haya ndio maisha ya mtu ambaye amejazwa na Roho Mtakatifu.

Biblia inasema kwamba, “Msiwachokoze watoto wenu.” Hili ndilo linafaa kuwa jambo la kwanza ambalo linafaa kuongoza matendo yetu juu ya watoto wetu. Hatuezi kamwe kutekeleza nidhamu sawasa ikiwa hatujajifunza kuwa watu wenye kiasi wenye kujua kutuliza hasira zetu. Wale ambao wamejazwa na Roho huwa ni watu wa kiasi. Unapokuwa unamwadhibu mtoto wako lazima uhakikishe kwamba huongozwi na hasira. Ikiwa utamwadhibu mtoto wako ukiwa unaongozwa na hasira, ukweli ni kwamba utamwumiza mtoto wako vibaya. Kwa njia moja utakuwa unatekeleza nidhamu ambayo wewe mwenye huna. Ili uweze kuwasaidia wengine, lazima kwanza wewe mwenyewe uwe ni mtu mwenye kiasi na kujua kutuliza hasira yako. Kwa hivyo hatua ya kwanza katika kuweka nidhamu katika maisha ya watoto wetu, lazima sisi wenyewe tuhakikishe kwamba tuko na nidhamu katika akili zetu na katika matendo yetu. Ni wakati huo tutaweza kutekeleza nidhamu kwa uangalifu na kwa hekima.

**Pili, ni lazima tuhakikishe kwamba sisi si watu wa kubadilika-badilika.**

Ikiwa mzazi yeyote atatekeleza nidhamu ambayo itamsaidia mtoto wake, lazima ahakikishe kwamba yeye si mtu wa kubadilika-badilika. Ninaposema hivi inamaanisha kwamba usiwe mtu ambaye hajulikana leo tabia yako itakuwa namna gani. Yaani wewe hisia zako zinabadilika kila wakati na unakaa kama mtu ambaye hana msimamo wowote. Hili ni jambo ambalo litamletea mtoto wako huzuni sana. Yaani wewe kuna wakati unacheka na hata kumpa nafasi mtoto wako ya kucheza. Lakini wakati mwingine wewe ni mtu mkali na hutaki kumwona mtoto akicheza. Hii itamletea mtoto wako ukosefu wa furaha katika maisha yake. Ikiwa wewe ni mzazi wa aina hii, itakuwa vigumu sana kutekeleza nidhamu ambayo itamsadia mtoto wako katika maisha yake yote. Mtoto wako hatakuheshimu hata kidogo.

Hapa simaanishi tu mtu mwenye hasira, baali hata tabia ya maisha. Mzazi ambaye anabadilika-badilika hawezi kumsaidia mtoto wake. Mzazi ambaye leo anafanya hili na kesho anafanya kinyume kabisa na jana, yeye hawezi kamwe kudumisha nidhamu ya kweli. Ni lazima mzazi ahakikishe kwamba yeye ni mtu ambaye habadiliki-badiliki katika maneno yake, na tabia yake, kwa sababu mtoto wake huwa anamwona kila wakati. Usiwaze kwamba haelewi na au anapuuza kile ambacho anakiona. Ikiwa mzazi anamkataza mtoto jambo fulani, lakini mtoto anamwona akilifanya jambo hilo, mtoto huyu hataheshimu maoni yake kwake.

**Tatu, lazima uhakikishe kwamba unamsikiliza mtoto wako vyema kabla ya kutoa uamuzi wa kumwadhibu mtoto.**

Litakuwa ni jambo la kumkasirisha mtoto ikiwa anaona kwamba nidhamu au adabu ambayo anapewa si ya kweli na haimfai kabisa. Ni jambo baya sana kwa mzazi ambaye hamsikilizi mtoto wake kwanza au hampi nafasi ya kujieleza kuhusu jambo. Kuna wazazi ambao kwa sababu ya tamaa ya kuadhibu mtoto, wamekosea watoto wao sana na kuwaumiza ilhali hawana makossa. Pia kuna wale ambao wanapeana adabu kali sana ambayo ni zaid ya makossa ambayo watoto wao wamefanya. Wengine pia hawafikirii juu yay ale ambayo wamesikia juu ya watoto wao, wao wanaadhibu kwa haraka. Labda yale wamesikia juu ya mtoto yalikuwa ya uongo au ni wao wenye walipuuza jambo Fulani na katika hali hizi zote, mtoto hapewi na nafasi ya kujieleza mwenyewe.

Ninajua kwamba kuna wale ambao watasema kwamba mtoto akiachwa ajieleze huenda hatapa nidhamu afayo. Kile ninasema ni kwamba katika kutia nidhamu, tusiwe wepesi bali tuhakikishe tunafahamu kila jambo vyema kabisa kwanza. Mpe nafasi mtoto ajieleze, na kama hatasema ukweli, basi unaweza kuadhibu lakini hata hivyo kwa njia ambayo inamfanya mtoto aelewa ni kwa nini anadhibiwa. Lakini ikiwa tutakataa kuwasikiliza watoto wetu, na tuendelee kuwadhibu bila makossa, basi tutakuwa tunakeleza nidhamu kwa njia mbaya sana na huenda hata hatutasaidia watoto wetu hata kidogo. Badala yake, watoto wataanza kuwa wenye kiburi dhidi yetu.

**Nne, tuhakikishe kwamba hatuadhibu watoto wetu kwa njia ya kuwaumiza.**

Hii ni hatari kubwa ambayo wazazi wengi leo wanakumbana nayo katika majukumu yao ya kutekeleza nidhamu juu ya watoto wao. Hatari ambayo wanakumbana nayo ni kuadhibu vibaya sana watoto wao. Hatufai kuwa wakatili kwa watoto wetu, bali tunafaa kuadhibu kwa upendo na kwa nidhamu.

Ninapomalizia ninataka kusema haya. Tunafaa kuadhibu kwa upendo na kama hatuwezi kuadhibu kwa upendo, afadhali kuacha kuadhibu. Hii inamaanisha kwamba kabla ya kuadhibu, tunastahili kuwa na nidhamu sisi wenyewe. Biblia inahimiza kwamba tuzungumze ukweli kwa upendo. Ndipo tuweze kutekeleza nidhamu sawasa, lazima tuwe na upendo. Tuwaadhibu watoto kwa sababu tunawapenda na si kwa sababu wanastali kuadhibiwa. Kitabu cha Waefeso kinatufunza kwamba, "Tena msilewe kwa mvinyo, ambamo mna ufisadi; bali

mjazwa na Roho" (Waefeso 5:18). Je, tunda la Roho ni gani? "Upendo,furaha, Amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole, kiasi" (Wagalatia 5:22-23). Ikiwa mzazi amejazwa na Roho na una hili tunda, nidhamu litakuwa jambo rahisi sana la kutekeleza. Lazima uwe na mtazamo mzuri kuhusu watoto wako na kwamba ufahamu kwamba hawa watoto ulipewa na Mungu uwalinda na uwashughulikia. Kusudi la Mungu kukupa watoto hao ni kwa sababu anataka uwalinda na kuwaonyesha njia ya kuja Kwake kupitia kwa Kristo Yesu. Wewe mzazi unajukumu la kuhakikisha kwamba unawaongoza watoto kumjua Mungu jinsi amejidhihirisha katika neno lake,. Kwanza ndipo uwaongoze, wanapaswa kuona maisha ya Mungu katika maisha yako mwenyewe. Ikiwa hawaoni maisha ya Mungu ndani mwako, hata uwaadhibu namna gani, hawatawahi kukuheshimu.

## KUWAFUNDISHA WATOTO JINSI WANAPASWA KUKUA

### Philip Doddridge (1702-1751)

**Watoto wanapaswa kufundishwa kuwatii wazazi wao.**

Hii ni amri ya Mungu ambayo amewaahidi wale wote ambao watatii,s kwamba wao watakuwa na maisha marefu (Kutoka 20:12). Mwandishi wa kitabu cha Waefeso anaandika akisema kwamba hii ndio amri ya kwanza ambayo ikon na ahadi. Hii inaonyesha kwamba Mungu amempa mzazi mamlaka ya kuhakikisha kwamba anamlea na kumsfundisha mtoto mambo muhimu ya maisha. Kwa sababu hii, watoto wanapaswa kufundishwa kwamba ni Mungu ambaye amewaweka katika maisha na mikono ya wazazi wao. Pia wanapaswa kufundishwa kwamba kuwatii wazazi wao ni jambo ambalo Mungu anawaamru walifanya. Kwa hivyo ikiwa watawatii wazazi wao, watakuwa wamemtii Mungu na ikiwa watakata kuwatii wazazi wao, basi watakuwa wamekata kumtiii Mungu. Kwa sababu hii, wazazi hawapaswi kuwafanya watoto wao kuwa wenye kiburi juu yao. Ikiwa watafanya lolote ambalo litawafanya watoto wao wenye kiburi juu yao, basi watakuwa wamekosa kuwaelekeza katika njia ya kweli. Hatufai kuwaachilia watoto wetu kufanya uamuzi katika maisha yao bila kuongozwa nasi, haswa wakati wao bado ni wadogo. Biblia inafundisha

kwamba, “Fimbo na maonyo hutia hekima; Bali mwana aliyeachiliwa himwaibisha mamaye” (Mithali 29:15). Kuhusu utiifu na upendo Biblia inasema, “Ni vema mwanadamu aichukue nira wakati wa ujana wake” (Maombolezi 3:27).

**Watoto wanapaswa kufundishwa kuwaheshimu na kuwajali watu wote.**

Katika kitabu cha Warumi tunasoma kwamba, “Pendo halifanyii jirani neno baya; basi pendo ndilo utimilifu wa sharia” (Warumi 13:10) na kwamba kila jambo linakamilishwa katika hili neno moja; pendo. Huu ndio upendo ambao tunafaa kuwafundisha watoto wetu, kuwapenda na kuwaheshimu watu wote. Ikiwa tutawafundisha upendo huu, basi hiyo ndio itakuwa sheria ya kuwaongoza katika maisha yao yote. Biblia inasema kwamba, “Basi yote yote mkatakayo mtendewe na watu, nanyi watendeeni vivyo hivyo, maana hiyo ndiyo torati na manabii” (Mathayo 7:12). Hivi ndivyo inapaswa kuwafundisha watoto wetu na tunafaa kuchunguza maisha yao kulingana na mstari huu. Tunafaa kuwasisitizia kwamba dini ya kweli inajumlisha kuwafanyia wengine mema na kwamba Mungu mwenyewe ni Mungu wa huruma na mwenye matendo mazuri na kwamba kila mtu ambaye ameokoka anapaswa kumfanyia mwingine mema Mungu anapopeana fursa la kufanya hivyo.

Tunafaa kuwafundisha watoto kwa maneno ambayo yanadhibitisha upendo na heshima kwa watu wote na wakati huo huo kuzuia lolote ambalo litakuwa kinyume na mafundisha ambayo tunawafundisha. Tunafaa kuhakikisha kwamba wao si wakatili na kutojali wengine. Tunafaa kuwakataza kwamba wasiwe watu ambao tabia yao ni kama ya wanyama. Pia tuwafundishe kuwapenda na kuwashughulikia wanayama wa wanyumbani kwa njia mzuri. Biblia inasema kwamba, “Mwenye haki huufikiri uhai wa mnyama wake” (Mithali 12:10).

Pia tukumbuke kuwafundisha kwamba hawafai kuwa watu wenye hasira, badala yake tuwahimize kusaidia wengine katika yale ambayo ni mazuri kufanya. Tuwafundishe kuwapenda na kuwasidia wale ambao ni maskini. Mungu amesema katika neno lake kwamba amebarikiwa yule ambaye anawajali maskini, naye Mungu atamkumbuka siku ya taabu zake. Pia Biblia iansema kwamba yule ambaye anawahurumia maskini, huyu anamkopesha Mungu na kile ambacho amempa Mungu, atarudishiwa. Tunafaa kuwaonyesha kwa tabia yetu kwamba kweli sisi tunaamini ahadi hizi za Mungu. Tuwahimize watoto wetu kuwa na tabia ya kuwasaidia wengine kila wakati bila kukoma. Ikiwa watoto

wetu tutawalea katika njia hii, basi tutakuwa tunawasaidia kufahamu na kuelewa ukristo wa kweli ni ukristo wa aina gani.

**Watoto wanafaa kufundishwa kuwa waangalifu.**

Ili linafaa kuwa jukumu letu ikiwa kweli tunajali mwili na nafsi za watoto wetu. Wao wanahitaji kuongozwa katika kila hali ya maisha yao ikiwa wao watakuwa watu wenye kumakinika, wenye bidii, watu wenye aungalifu na wenye heshima. Biblia inasema, "Je, wamwona mtu mwenye bidii katika kazi zake? Huyo atasimama mbele ya wafalme; Hatasimama mbele ya watu wasio na cheo" (Mithali 22:29). Ni ukweli kwamba wale ambao wanajihushisha na kufanya kazi kwa bidii, wao hujiepeusha na dhambi na taabu nyingi. Lakini wale ambao wanakaa tu na ni wa nyonge katika kazi zao, wao huanguka sana katika majaribu na dhambi nyingi kwa sababu ya uzembe wao.

Kwa hivyo mzazi ambaye ameokoka, anafaa kuwa mwangalifu kwamba watoto wake hawaanguki katika dhambi ya uzembe wala hawafuatani na watu ambao ni wazembe. Yeye atahakikisha kwamba watoto wake wanajihusisha na kazi na kwamba wanapendezwa na kufanya kazi. Badala ya watoto wako kutembea huku na kule jinsi vijana wengi leo wanavyofanya, mazazi anapaswa kuwapatia kazi ya kufanya. Wakati unawapatia kazi, pia kumbuka kwamba usiwapatia kazi ambayo ni ngumu sana, kwa sababu wao bado ni watoto, kwa hivyo wapimie kile wanaweza ili miili yao isiumia. Usiwaze kwamba watoto wako hawawezi kufanya chochote. Kwa kawaida, watoto ni watu ambao wanapenda kufanya kazi na kujua mambo mengi sana. Wakati wanafanya jambo huwa wanapenda kuonyesha kwamba kweli wao wamejua. Ni furaha yao kufanya kazi. Pia wakati wamefanya kazi kuwa mtu wa kuwahimiza. Wapongeze na wafurahia, kwa njia hii unaendelea kuwahimiza kufanya kazi. Pia kwa njia hii, unawatayarisha kwa ajili ya maisha yao ya badaye.

**Watoto wanapaswa kufundishwa kuwa watu waaminifu.**

Kuwa mwaminifu ni jambo la maana sana katika maisha ya mkristo. Ni jambo la huzuni sana kuona jinsi dhambi inavyojitokeza katika maisha ya watoto wetu. Biblia inasema kwamba kutoka katika tumbo sisi ni wenye dhambi na tunazungmza uongo (Zaburi 58:3). Kwa hivyo tunafaa kuwa waangalifu sana kuhakikisha kwamba watoto wetu wanajua ukweli wa neno la Mungu. Wanafaa kujua kwamba wao ni wenye hatia machoni pa Mungu kwa sababu ya dhambiz zao. Kwa

sababu hii, tunafaa kuhakikisha kwamba hatuwaongozi watoto wetu katika dhambi. Tuhakikisha kwamba hatuwaogopeshi au hatuwalazimishi katika jambo, kwa sababu hii inaweza kuwafanya wadanganye kwa sababu tunataka ukweli kutoka kwao. Pia tuhakikishe kwamba kabla hatujawaadhibu, tunafanya upelelezi wa kutosha ili tudhibitishe jambo kabla ya kufanya uamuzi wowote. Kwa njia hii, tutakuwa tunawalinda watoto wetu dhidi kuongozwa katika majaribu ya dhambi kama kudanganya. Ikiwa tunapata kwamba watoto wetu wamedanganya, basi tunapaswa kuwaeleza hatari ya maneno yao ya uongo na kuwakemea na kuwarekebisha mara moja. Hata wakati mwingine kuwaadhibu, ili wajui hatari ya makosa yao. Ni lazima tuwaonyeshe watoto wetu kwamba dhambi yoyote ni mbaya machoni pa Mungu. Ikiwa tutajitahidi katika kuleta ukweli katika maisha yetu, basi tutawasaidia sana watoto wetu kuwa watu waaminifu.

Wakati tunawakemea juu ya kusema uongo, basi pia tunapaswa kuhakisha kwamba tunawakemea katika tabia za kitoto za dhambi. Kila wakati tuwakumbushe kuhusu kile ambacho Biblia inasema: “Aendaye kwa unyofu huenda salama; Bali apotoshaye njia zake atajulika” (Mithali 10:9). Kila siku usichoke kuwaonyesha uzuri na faida ya kuishi maisha amabyo ni ya uaminifu. Pia waonyeshe hatari ya kuishi maisha ambayo ni udanganyifu. Ikiwa wataenenda katika maisha haya, basi wao watakuwa wanajitengenezea maisha mabaya sana. Zaidi ya yote tuwakumbusha kwamba Bwana Yesus Kristo anapendezwa na maisha ya unyofu na haki na kwamba Yeye huwaongoza wale ambao wanaishi maisha ya haki; wale ambao wanadanganya ni chukizo sana kwake. Biblia inasema kwamba, “Bali waonga, na wasioamini, na wachukizao, na wauaji, na wazinzi, na wachawi, na hao waabuduo sanamu, na waongo wote, sehemu yao ni katika lile ziwa liwakalo moto na kiberiti” (Ufunuo 21:8).

### Watoto wanapaswa kufundishwa unyenyekevu.

**H**ili jambo ambalo tunajifundisha kutoka kwa Bwana wetu Yesu Kristo. Yeye Kristo hangenyenyekea, basi hangeweza kutuletea wokovu. Biblia inasema kwamba, “Kumcha Bwana ni maonyo ya hekima; Na kabla ya heshima hutangulia unyenyekevu” (Mithali 15:33). Yule ambaye anajiinua yeye hunyenyekezwa na yule ambaye anajinyenyekeza huinuliwa na Mungu na wanadamu.

Kwa hivyo ili tuweze kuwasaidia watoto wetu, lazima tuhakikishe kwamba tunawaonya juu ya kiburi katika maisha yao. Kiburi ndicho kilisababisha Adamu na Hawa kuanguka katika dhambi. Kwa kawaida

kila mwanadamu amezaliwa akiwa na kiburi kwa sababu sisi sote tumetoka katika Adamu. Lakini sasa hii haimaanishi tuendelee katika kiburi. Biblia inatuambia kwamba tuepuke dhambi, tuache dhambi. Tuwafundishe watoto wetu kuwa wenye unyenyekevu na kuwaheshimu watu wote.

Wanafaa kuwaheshimu wale ambao ni umri kuliko wao. Hata wakati mwingine wanafaa kunyamaza wakati watu fulani wanazungumza haswa wale ambao ni wazee kuwaliko. Ni lazima wajifundishe kudhibiti ulimi wao ambao ikiwa wanautumia vyema, wao watahesabiwa wenye hekima hata wakati mwingine kuwaletea amani na heshima katika maisha yao.

Pia wanafaa kuhimizwa kwamba hawapaswi kuwa wenye kiburi kwa wale ambao ni wa mri wao. Lakini tuwafundishe kunyenyekea hata wakati mwingine kukubali kudharauliwa kwa ajili ya amani. Wanapaswa kuheshimiana na wale ambao ni wa umri wao na kuwaheshimu wote. Ninajua kwamba haya yanaonekana kuwa mambo magumu kwao, lakini ukweli ni kwamba haya ndiyo mambo ambayo yanapaswa kuzingatiwa na wanadamu wote ikiwa wanataka kuishi maisha ya amani na watu wote.

**Watoto wanapaswa kufundishwa kujitolea katika maisha yao.**

Bila kujitolea, hatuwezi kamwe kumfuata Yesu au kuwa watu wake na pia hatuwezi kuendelea katika maisha ya humo ulimwenguni. Katika kila jambo ambalo mtoto anapanga, ni lazima ajue kwamba kuna mambo katika maisha ambayo yanaweza kufanyika na kutatiza mawazo yetu na kushusha mioyo yetu na kukatiza mapenzi yetu. Kwa hivyo tunapaswa kuwafundisha ukweli huu na ikiwa tutafaulu kuwafundisha, basi tutakuwa tumewasidia sana kuwa wenye hekima.

Ikiwa mtu ana tama asana ya kufanya jambo fulani, mara mingi huwa wapotelea katika tamaa hii na kuanguka katika dhmabi. Ujumbe wa Injili, hutufundisha kwamba, tunapaswa kuishi maisha ya ukweli, ya haki na maisha ya kumcha Mungu. Kwa hivyo watoto wanapswa kufundishwa kuishi kwa ukweli na wanapaswa kuelezwa kwamba lazima wawe tayari kujitolea. Ikiwa tamaa zao ndizo zitawaelekeza kupata kile ambacho wanataka, basi ni wazi kwamba wengi watayaharibu maisha yao kwa sababu mambo mengi ambayo huwa wanayatamani ni mabaya kwao. Mara nyingi kwa sababu ya upedno wa kina mama wa kuwaacha watoto wao wafanye jinsi wanataka, ndio imewafanya watoto wengi wapate shida nyingi katika maisha yao. Ni

hekima na upendo kuwanyima watoto vile ambavyo wanavitaka pia kutowaharibu na vitu vya ulimwengu huu kama vyakula na mavazi. Ni lazima watoto wajue kwamba kuna wakati ambapo maisha yanakuwa magumu na wakati ambapo kuna na furaha. Ni lazima wajue na wajifundishe kukumbana na kila hali ya maisha; wakati chakula kiko na wakati hakuna chakula.

Ni vizuri kwamba watoto wetu wakati fulani tunawanyima vitu fulani si kwa sababu tunawachukia bali kwa sababu tunataka kuwafundisha jinsi wanapaswa kuishi katika maisha yao ya mbeleni. Kwa njia hii watoto watajifundisha kujima na hekima katika maisha yao.

# MAMBO AMBAYO YANAZUIA MZAZI KUWALEA MTOTO KATIKA KRISTO

## John Angell James (1785-1859)

Ni huzuni kwamba wengi wa wazazi ambao wameokoka, wametumia njia fulani fulani za kuwalea watoto wao katika Kristo, lakini hawajafaulu. Katika mafundisho haya sifundishi kuhusu jamii hizi, ambazo zinaonekana kumjua Mungu. Mahali ambapo hakuna maombi ambayo yanasikika na wazazi hawawafundishi watoto wao neno la Mungu. Wazazi hawa wamepuuza kabisa amri ya Mungu kwao na wamepuuza nafsi za watoto wao hata kama wao wanakiri kumjua Mungu. Kwa sababu ya kutotii amri ya Mungu katika maisha yao, watoto wao wamegeukia dunia. Kuna vijana wengi ambao ninawajua ambao wametoka katika manyumba haya. Wao wanajua kabisa ukristo na ni wabaya sana kuliko wale ambao wanatoka katika jamii ambazo hazikiri kumjua Mungu au kuokoka. Kwa sababu ya unafiki wao na maisha ya kutojali, watoto wao hawamweshimu Mungu kamwe na wamejiweka mbali sana na dini ya ukristo.

Ninataka kuzungumza juu ya mafundisho ya ukristo ambayo yameonekana kutoleta mabadiliko yoyote katika maisha ya watoto. Kuna wakati ambapo tunawaona watoto ambao wemeombewa wakiwa katika vikundi vibaya sana. Sisemi kwamba ni makossa ya kila mzazi ambaye ana mtoto ambaye anaishi maisha ya kutomtii Mungu. Sitaki

kumwongezea huzuni mzazi yeyote ambaye anahuzunika kwa sababu ya tabia ya mtoto wake. Ninajua kwamba katika hali fulani fulani, si wazazi wa kulaumiwa, bali ni mtoto mwenyewe. Mtoto anaweza tu kubadilika si nnguvu za mzazi bali, kwa kazi ya Roho Mtakatifu katika moyo wake. Ni Roho Mtakatifu ambaye anaweza kumfanya mtoto ahuzunike kwa sababu ya dhambi zake. Kuna wazazi ambao wajitolea sana katika kuona kwamba watoto wao wanamjua Kristo na wanaokoka, lakini baadaye wamepata kwamba watoto wao wameendelea katika kutotii neno la Mungu. Biblia inafundisha kwamba Mungu anatawala kila kitu na kwamba anamhurumia yule ambaye anataka kumhurmia (Warumi 9:15). Lakini hata hivyo, kuna mwelekeo mzuri katika kuwafundisha watoto neno la Mungu ambao unaweza kuleta mazao mema katika maisha ya watoto wetu. Mungu huwa anabariki mwelekeo huo ambao unaambata na neno Lake. Biblia inasema kwamba, "Mlee mtoto wako katika njia impasayo, Naye hataiacha, hata atakapokuwa mzee" (Mithali 22:6). Huu ni ukweli.

Ninataka tutazame mambo ambayo yanamzuia mzazi skuwalea watoto katika Kristo.

**Wengi hata kama wanaendelea kufundisha watoto neno la Mungu, huwa hawafanyi jambo hili kwa mioyo yao yote wakitarajia matokeo mema.**

Ni ukweli kwamba kama tutaendelea kufundisha watoto wetu neno la Mungu, tunapaswa kufanya jambo hili kwa mioyo yetu yote na kila wakati. Hatufai kulifanya kwa njia ambayo mioyo yetu haina furaha au kwa sababu hatuna mambo mengine ya kufanya. Tunapaswa kulifanya kwa miyo yetu yote tukimwomba Mungu kwamba atawaokoa watoto wetu. Mzazi anapaswa kutenga muda kila siku kuwafundisha watoto wake neno la Mungu. Yeye anapaswa kutekeleza majukumu yake yote kama mzazi kwa njia ambayo inamletea Mungu utukufu. Baba anapaswa kuogoza nyumba yake kila siku katika kusoma Biblia na kuomba. Mama naye anapaswa kuingilia na kusaidia katika kuwafundisha watoto nyimbo za kikristo na misingi ya ukristo. Ikiwa mambo haya yote, hayatafanywa kwa kusudi moja ambalo ni kuona kwamba watoto wanaokoka na kuishi maisha yao kwa ajili ya Kristo, basi hatutawafaidi watoto wetu kiroho hata kidogo. Kukosa kujitolea kabisa kwa mioyo yetu katika kuwafunza watoto wetu neno la Mungu, itawafanya wachukia dini ya ukristo badala ya kuipenda.

Mafundisho ya Biblia katika nyumba yanapaswa kufanywa kila siku na kila wakati. Yanafaa kuzingatia sehemu ya maisha; maisha ya shule,

marafiki, burudani na vitabu ambavyo mtoto anapaswa kuvisoma. Ikiwa tutafundisha tu watoto lakini mafundisho hayo hayatilii maanani maisha ya kila siku ya mtoto, basi hatutakuwa tunasaidia watoto wetu sana. Ikiwa mkulima anatupa-tupa mbegu na hazipandi kwa mpangilio na kuwa uvumilivu sana, hazitaleta mazao mazuri kama zile ambazo zimepandwa kwa mpangilio mzuri na kuwa uvumilivu sana. Ikiwa mzazi hajajitolea kwa moyo wake wote, basi pia astarajie mtoto wake awe amejitolea kwa kumsikiliza na kutiii. Ikiwa baba ya mtoto nia yake sana ni mtoto wake afanye vizuri katika masoma yake lakini si kwamba mtoto wake aokoke, au mama anapenda sana msichana wake ampate bwana tajiri kuliko jinsi anavayomtakia mtoto wake aokoke, basi wanaweza kufundisha Biblia watoto wao lakini mioyo yao haitakuwa katika mafundisho hayo na kwa hivyo wasitarajie kuona mtoto akiokoka. Mtoto anaweza kuwa mtu mzuri na kuonekana kujua mambo ya dini lakini yeye hatakuwa mwana na Mungu. Ikiwa kweli tutawafundisha watoto wetu neno la Mungu, ikiwa mioyo yetu na mapenzi yetu ni kuona kwamba wanaokoka na kuishi maisha matakatifu, basi Mungu atatubariki kwa kuwaokoa watoto wetu. Huu ndio unafaa kuwa moyo wa kila mzazi ambaye anamfundisha mtoto wake neno la Mungu.

**Kukosa kutilia maanani nidhamu katika maisha ya watoto wako ni jambo linguine ambalo ni ckizuizi kwako kumlea watoto wako katika Kristo.**

Mzazi amepewa mamlaka na Mungu katika maisha ya mtoto wake na kwa hivyo anapaswa kutumia mamlaka hayo kwa njia ambayo inamletea Mungu utukufu. Kila mzazi ni mtu ambaye anapaswa kuhakikisha kwamba sheria ya Mungu inadunishwa katika jamii yake. Yeye anapaswa kuwazuia watoto wake kuenenda katika njia ya dhambi, anapaswa pia kuwaadhidbu na watoto nao wana jukumu la kutii. Mzazi anapaswa kuhakikisha kwamba watoto wake wanaenda katika njia amabazo zinamletea Mungu utukufu. Yeye anafaa kuwakemea wakati wanaenda katika njia mbaya. Yeye anapaswa kuwaongoza watoto wake kusoma vitabu ambavyo vinawafaidi kiroho, yeye anapaswa kuwaongoza juu ya aina ya marafiki ambao wanapaswa kuwa nao na jinsi wanapaswa kumaliza muda wao. Ikiwa anaona kwamba watoto wake wanaenda katika njia kinyume na jinsi anavyowafundisha, anapaswa kutumia mamlaka yake katika maisha yao na kuwakemea na kuwakataza. Mzazi hafai kuwa kama Eli ambaye aliwaona watoto wake wakimwasi Mungu lakini alizungumza tu na wao: “Mboma mnatenda

mambo kama hayo? Maana nasikia habari za matendo yenu mabaya kwa watu hawa wote." (1 Samweli 2:23). Anapaswa kutawala nyumba yake na watoto wake kufahamu kwamba yeye anahitaji kutoka kwao utiifu. Lakini anapaswa kufanya hivi yeye mwenyewe akiwa mfano kwa watoto katikas ya uhusiano wake na Mungu.

Nyumba nyingi zinaharibika kwa sababu ya ukosefu wa nidhamu kwa watoto katika manyumba hizo. Ikiwa mkulima anatarajia mazao mazuri, ni lazima ahakikishe kwamba kila wakati analichunga shamba lake na anangoa magugu ambayo yanajitokeza kila mara katika shamba hilo. Asipofanya hivi, basi ni wazi kwamba yeye hataona mazao mazuri katika shamba hilo. Kwa hivyo mzazi anaweza kuweka nidhamu mzuri katika nyumba yake, lakini asipokuwa makini kuondoa tabia mbaya, hasira na dhambi miongoni mwa watoto wake, basi ni wazi kwamba hatakuwa amesaidia sana watoto wake. Yeye anaweza kuwa mchungaji mzuri na baba mzuri lakini asipokuwa mfalme katika nyumba yake, mambo mengi yataenda vibaya sana. Ikiwa akina baba watapuuza majukumu yao ya kuwalea watoto wao katika nidhamu na maonyo ya Bwana, basi wao wasitarajie watoto wao kukua katika njia za Bwana na katika nidhamu mzuri. Ikiwa katika nyumba nidhamu haifuatiliwi kikamilifu, kwa mfano ikiwa wakati fulani baba ni mwangalifu sana katika mambo ya nidhamu na wakati mwingine kwa sababu hataki watoto wamwogopi, anapuuza nidhamu hiyo, basi atapata kwamba pole pole atakuwa anapuuza majukumu yake kwa watoto wake na watoto wake watamzoea hivyo na itakuwa vigumu sana kuwaongoza vyema.

Katika hali fulani fulani, nidhamu huwa inatekelezwa kwa haraka sana na katika hali zingine, nidhamu inachelewa sana. Ni rahisi katika jamii kufanya mzazi na mtoto kuzoeana kiwango kwamba hata heshima inapungua kati ya mzazi na mtoto. Ni vyema kabisa kuwaonyesha na kuwaeleza watoto wetu kwamba ni jukumu lao kwa Mungu kuheshimu wazazi wao. Ikiwa watakuwa watu wazima wakiwa hawaheshimu wazazi wao, hawatawahi kumheshimu mtu yeyote. Watoto wanapokuwa chini ya wazazi wao, ni lazima wawatii wazazi kwa vyovyote vile. Kuna wazazi ambao huwa wanaacha kuweka nidhamu katika maisha ya watoto wao kwa sababu wanaona kwamba watoto hao wanakuwa wakubwa. Utasikia mzazi akisema kwamba, "huyu ni mtu mkubwa wacha afanye kile anataka shauri yake." Ni jambo la huzuni kuona kijana au msichana mdogo akiwa na kiburi juu ya wazazi wake kiwango kwamba hata mzazi hawezi akamwambia lolote. Ikiwa watoto wetu tutawafundisha kutii kwanza wakiwa wadogo, basi litakuwa jambo rahisi sana kwao hata wakati wanakuwa watu wazima. Ikiwa mzazi anaona tabia fulani katika

maisha ya mtoto wake, anapaswa kushughulika nayo hapo na hapo ili aweze kumsaidia mtoto wake. Mtoto anapaswa kumheshimu na kumtii mzazi wake si kwa sababu mzazi atamchapa kiboko, bali kwa sababu wewe mzazi umemfundisha mtoto wako jinsi anapaswa kuishi maisha yake akiwa chini ya uongozi wako kama mzazi wake.

**Hutuwasidia watoto wako kiroho kwa sababu wewe ni baba mkali sana na kwamba kwa nyumba kila mtu anakuogopa.**

Kuwa mkali sana kumeharibu maisha ya watoto wengi sana kama tu kupuuza nidhamu imeharibu maisha ya wengi pia. Kuna wengi ambao wanasema kwambna wanawapenda sana watoto wao, na kwa hivyo hawawezi kuwaadhibu. Ni ukweli kwamba mawazo ya mwanadamu huwa ni mepesi kuonyesha huruma. Upendo ni jambo muhimu sana katika maisha ya mzazi, na hata wale ambao wanaonekana kuwa wakali, bado pia wao wako na upendo. Tukisoma katika Biblia mfano wa mtoto aliyepotea, ni mfano ambao unatuonyesha nguvu za upendo. Ikiwa baba atakuwa mtu ambaye aanaongoza nyumba yake bila upendo, ikiwa atatia nidhamu katika watoto wake bila upendo, ikiwa yeye ni mtu wa kupiga makelele tu na tabia yake inawafanya watoto wajihisi kwamba wao ni kama watumwa, mioyo ya watoto wake itajawa tu na uoga wala si heshima kwake. Wao watakuwa wanamtii si kwa sababu yeye ni baba yao, bali kwa sababu ya uoga kwamba atawaumiza. Watoto wake watakuwa wanamdanganya ili waepuke kuadhibiwa. Baba wa aina hii, yeye ni mtu ambaye anaondoa furaha katika maisha ya watoto wake. Utapata kwamba akiingia katika nyumba yake, ikiwa watu walikuwa wanacheka, kila mtu ananyamaza na kuanza kuondoka. Yeye ni mtu ambaye hana uhusiano wowote na watoto wake. Tabia ya baba kama huyu haiwezi kamwe kuwaongoza watoto wake katika kumjua Mungu na dini ya ukrlsto. Yeye hawaachi na tamaa yoyote ya wokovu kwa sababu kile ambacho anawadhibitishia katika maisha yao, si tabia ya Mungu.

Baba wa aina hii, hana haja ya kuwafundisha watoto wake neno la Mungu. Yeye kazi yake ni kuogopesha watoto wake na kufanya mioyo yao iwe migumu sana dhidi ya dini ya ukristo. Yeye anawafanya wajichukie na kujihurumia sana. Yeye huwafanya watoto wake wakose tamaa ya kuishi naye. Yeye pia anawafanya wawe na tamaa ya kutaka kujitawala kwa sababu wanaona kwamba ni kwa njia hiyo pekee wanaweza kuwa huru, na hii itawaongoza kupotelea katika dhambi.

Ninasihi kila atekeleze nidhamu katika maisha ya watoto wake kwa upendo. Wao wanapaswa kuishi maisha matakatifu na kutia nidhamu

kwa njia ambayo inawahimiza sana watoto wao na wala si kuwafanya wachukia maisha yao. Wanapaswa kuwaonyesha kwamba sheria ambayo wanaifuata ni sheria takatifu na ni ya haki na nzuri na kwamba kuitii ni kupata Baraka.

**Ukosefu wa ukakamavu katika maisha ya wazazi ni moja wapo wa vizuizi katika kuwale watoto katika Kristo.**

Je, wazazi wanapaswa kushawisha na nini ili waweze kuwa wakakamavu katika majukumu yao? Kwa sasa ninatakuzungumza na wazazi ambao wameokoka. Maisha ya ukristo katika wazazi hawa, inaonekana na watoto wao kwa umbali kwa sababu ya ukosefu wa ukakamavu. Unapotazama maisha yao utapata kwamba kuna upendo wa ulimwengu na mitindo ya ulimwengu huu, hawaonekani kuwa wamejitolea kabisa kwa Mungu, hasira ya kila wakati, kulalamika kila wakati wanakumbana na shida za ulimwengu na uhasama ambao wanadhibitisha juu ya wakristo wenzao, haya mambo yote yanaonekana na watoto wao na kuwafanya watoto hawa waone kwamba ukristo hauna faida yoyote. Ukweli ni kwamba huenda heshima yao juu ya ukristo ipotea kabisa au ipunguke.

Ikiwa mzazi yeyote anataka adabu na maonyo ya Bwana yawafaidi watoto wake wakati anawaongoza, basi lazima mzazi mwenywe awe mfano bora kwa watoto wake. Haitoshi tu kusema kwamba wewe umeokoka au kuwaonysha wale ambao wameokoka kwa kweli wewe umeokoka. Unafaa kudhibitisha kwa watoto wake kwamba wewe umeokoka na kwamba maisha yako yote umejitolea kuishi kwa utukufu wa Mungu. Maisha yako ya utakatifu yanafaa kuwa lengo la juu. Kwa wazazi wote, himizo langu kwenu ni hili, sema machache kwa watoto wako kuhusu ukristo, lakini ishi maisha ya ukristo. Kuwa mwangalifu jinsi unavyoishi maisha yako kwa sababu watoto wako wanakuona. Kwa kusema hii simaanishi kwamba sasa wewe uwe mnafiki kwa sababu hata ukishi maisha ya unafiki, bado watoto wako watakuona na watajua wewe ni mnafiki. Kuwa mwangalifu usiwe mtu wa kuzungumza sana juu ya makosa ya wakristo wenzako na ikiwa utazungumza, wache iwe ni kwa sababu ya uzuri. Wazazi wengi wamechanganya watoto wao na kuwatia huzuni mwingi kwa kuzungumza juu mabaya ya wakristo wenzao. Hata wengine wamefurahia sana shida na taabu za wakristo wengine. Pia kuwa mwangalifu kwamba usizungumze mbele za watoto wako juu ya udhaifu au taabu za mchungaji wako. Badala yake, zungumza vyema juu yake na mafundisho yake ili watoto wako waendelee kuwa na moyo wa kumsikiliza na kufaidika kiroho kutokana

mafundisho yake. Wahimiza kuiga hata wakristo wengine katika tabia na mwenendo wa maisha. Waonyesha kwamba ukristo wa kweli unahitaji kuheshimika sana na wote. Kwa ufupi ni kwamba, kwa sababu mfano wako wa maisha unahitajika sana katika maisha ya watoto wako ili wahimizwa, kumbuka, "Basi, kwa kuwa vitu hivi vyote vitafumuliwa hivyo, imewapasa ninyi kuwa watu wa tabia gani katika mwenendo mtakatifu na utauwa" (2 Petro 3:11).

**Mtoto kubwa ambaye hajaokoka, huwa pia anachangia sana katika kuwa kizuizi katika kuwalea wale ambao ni wadogo wake.**

Watoto ambao hawajaokoka katika jamii huwa pia wako na ushawishi mkubwa sana katika maisha ya wale ambao bado ni wadogo. Hii ni kwa sababu wale ambao ni wadogo huwa wanawatazamia kuwafanyia mambo fulani fulani. Kuna wakati ambapo wanaweze kuja nyumbani na wako na vitabu au marafiki au vitu vya music au kuonwa kwa runinga ambavyo wataviona na wale ambao ni wadogo na hii inashawishi maisha ya wale ambao ni wadogo. Kwa hivyo ni vyema sana kwamba wazazi wanakuwa waangalifu sana juu ya watoto wao ambao wamekuwana hawajaokoa ili wasishawishi wale ambao ni wadogo katika njia ya dhambi. Ikiwa tabia ya wale ambao ni wakubwa ni mbaya sana kiwango kwamba itawatatiza wale ambao ni wadogo na kuwaongoza katika dhambi, basi ni wazi kwa ajili ya kulinda wale ambao ni wadogo, wakubwa wanapaswa kuonywa na hata kama hawasikii kuondolewa katika nyumba. Mtoto mmoja ambaye ni mwasi, anaweza kuwaongoza wengine wote katika njia mbaya ya dhambi. Haya ni mambo ambayo mimi mwenyewe nimeyaona na hata ninyi wasomaji wangu huenda mmeyaona pia. Ni ukweli kwamba si rahisi kumwondoa mtoto wako, lakini ikiwa yeye hasikii na tabia yake inawafanya wengine wawe wabaya, basi ni wazi kwamba lazima ataondoka. Ikiwa tutakuwa wakarimu kwa yule ambaye anawaharibu wengine, basi tutakuwa tunawakosea kwa wale ambao wanaharibiwa. Uovu ni kama ugonjwa ambao unasambazwa haswa ukiwa na mtu ambaye niwa karibu sana nawe. Kwa njia hiyo lazima tuhakikisha kwamba wale ambao wanataka kuambukiza wengine tunawaweka kandoo.

**Marafiki wabaya ambao watoto wetu wanatembea nao, pia wanakuwa kizuizi kubwa sana kuwalea watoto katika Kristo.**

Mzazi ambaye ameokoka, anapaswa kila wakati kuona ni kina nani ambao wanatembea na watoto wake. Hili ni jambo la muhimu sana kwa wazazi wote. Ikiwa mtoto wako ana rafiki mmoja ambaye ni mbaya,

huyu rafiki ataharibu kile ambacho unaweka katika maisha ya mtoto wako nyumbani. Ni ukweli kwamba si rahisi kujua ni nani mbaya au mzuri. Tangu wakati wakiwa watoto wafundishe kwamba ni vyema wakueleza ni marafiki wa aina gani ambao wako nao. Hakikisha kwamba wewe ni rafiki ya watoto wako wa kwanza, ili chochote kinachoenedelea katika maisha yao wao watakuwa wanakueleza. Usiwahi kubali marafiki ambao hawatawasaidia watoto wako kukuwa katika ukristo wao. Hili ni jambo ambalo tunastahili kuhiza sana katika maisha ya watoto wetu, haswa katika siku hizi mbaya sana. Ukitazama utaona kwamba vijana wengi leo wanaletwa pamoja na mambo mengi ambayo inapagwa na vikundi tofauti tofauti. Kama mzazi lazima uhakikishe kwamba mahali watoto wako wanainda haswa wakiwa na marafiki wako, ni mahali ambapo hapatawahimiza katika dhambi. Haitoshi tu kwamba marafiki wake au mahali anaenda ni mahali pa kufundisha Biblia. Lazima uhakikishe hata kama ni mafundisho ya Biblia, ni nani anafundisha na anafundisha nini. Haijalishi kwamba anaenda na wale ambao wanakuja kanisani, lazim tuwe waangalifu kwa sabau si wote ambao wanakuja kanisa tabia na mwennedo wao ni mzuri na ni wa kuhimiza katika maisha ya ukristo.

**Migawanyiko miongoni wa wakristo kanisa huwa ni kizuizi katika kuwalea watoto wetu katika Kristo.**

Watoto wetu huwa wanaona mengi ambayo ni kinyume na Biblia. Mambo haya huwa yanawasumbua sana katika akili zao. Ikiwa wanaona kwamba fulani au kikundi fulani katika kanisa hakipatani au hawapatani, huwa ni jambo baya sana. Hii huwafanya watoe akili zao kwa ukristo wa kweli kwa sababu ya tabia ambayo ni kinyume na neno la Mungu.

Kwa hivyo tunapaswa kila wakati kujichunga kwamba katika makanisa yetu, tunatatua mafarakano kwa njia ambayo inamletea Mungu utukufu na watoto wetu wanajifunza mengi kutoka kwa haya yote. Ni ukweli shida zipo katika makanisa na hili ni jambo ambalo tunapaswa kuwaeleza watoto wetu wajue, lakini pia ni lazima tujue kwamba shida hizi kuna njia ya kuzitatua katika Biblia. Kwa hivyo tuhakikishe kwamba tunatatua shida hizi kulingana na mafundisho ya Biblia.

**Maoni na tabia ya wengi ambao wanawaza kwamba majukumu ya msichana na kijana kwa wazazi wa tofauti.**

Wengi leo wanawaza kwamba watoto wako huru na kwamba wazazi wao hawapaswi kuwaeleza wanafaa kufanya nini. Mawazo kama haya ni ya uongo na si ya Biblia. Ikiwa watoto wataasi wazazi wao, basi hawafai kutarajia baraka kutoka kwa Mungu, kwa sababu ni Mungu ambaye amewapa wazazi mamlaka ambayo wako nayo katika maisha ya watoto wao. Watoto wao ambao wanaona kwamba kutii wazazi wao ni jambo gumu sana, hawatakuja kwa Kristo.

Haya ni mambo ambayo ninawaza kwamba yamekuwa kizuizi kwa wengi kuwalea watoto katika Kristo. Kwa hivyo msomaji wangu, waza juu ya mambo haya kwa uangalifu sana ili ufanye kile ambacho kinakubalika machoni pa Mungu. Jitolee kabisa katika kila jambo kuhakikisha kwamba unawalea watoto wako katika Kristo, na kwamba wanamjua Kristo na kuishi maisha yao kwa utukufu wake.

# HATARI YA WATOTO WASIOMCHA MUNGU

## Edward Lawrence (1623-1695)

Ni jambo la huzuni sana kwa waziza ambao ameokoka kuwa na watoto ambao hawamchi Mungu: "Azaaye mpumbavu ni kwa huzuni yake mwenyewe; Wala baba wa mpumbavu hana furaha" (Mithali 17:21); "Mwana mpumbavu ni msiba kwa babaye" (Mithali 19:13).

Tutaona mambo matatu kuhusu jambo hili.

### Uoga

Hili ni jambo ambalo linaleta shida sana kwa mzazi. Wazazi ambao wameokoka mara kwa mara huwa wamejawa na uoga kwa sababu ya watoto wao ambao ni waovu. Wao wanaogopa kwa sababu kila matu ambaye anakuja kwao huwa anawaletea habari mbaya kuwahusu watoto wao waovu.

Tutaona mambo matatu ambayo hawa wazazi huwa wanaogopa sana kuhusu watoto wao.

a). Wanaogopa kwamba huenda watoto wao wako katika dhambi mbaya sana.

Huu ndio ulikuwa uoga wa Ayubu wakati watoto wake walipokuwa washerekia pamoja. Ayubu alisema, "Yumkini kwamba hawa wanangu

wamefanya dhambi, na kumkufuru Mungu mioyoni mwao" (Ayubu 1:5). Watoto wa wazazi hawa mara kwa mara wao huwa hawako pamoja nao na kwa hivyo wanaogopa sana. Wanajuwa kwambna watoto wao kila wakati wanajaribiwa na shetani na vitu vya dunia na kutembea na watu waovu na kwamba mioyo yao huwa inakubali kufanya mambo haya yote. Wao wanajua kwamba watoto wao wamemkasirisha Mungu na kwa hivyo Mungu amewapeana katika tamaa zao. Kwa hivyo uoga wao ni wa kila wakati kwa sababu wanajua kwamba hawa watoto wao ni wadanganyifu, ni wenye kulaani, ni wazinzi, ni walevi na wanaendelea kujiharibu wakati huo huo wakiwaharibu wengine.

b). Wanaogopa kwamba huenda hukumku kali ya Mungu itawapatawatoto wako katika maisha haya.

Daudi aliogopa sana kwamba mtoto wake Absalomu asije akafa kataika vita kwa sababu ya dhambi zake. Wazazi hawa wanajua kwamba watoto wao wamemwasi Mungu na kwamba wao ni kama ndege ambao hawako katika vyota vyao (Mithali 27:8) na wako katika hatari kubwa sana. Wanajua nini Mungu anasema katika neno lake juu ya wale wote ambao wanaendelea katika uasi. Wanajua vyema kwamba hukumu ya Munfu itakuja juu ya maisha ya watoto wao ikiwa wanaendelea katika uasi. Kwa hivyo wanaogopa sana kwamba dhambi za watoto wao zitawafanya wafe kifo cha aibu sana.

c). Wanaogopa kwamba watoto wao watapotea milele jahanum.

Wanajua kwamba watoto wao ni watoto wa ghadhabu na kwamba wako katika dhambi ambazo Mungu ataangamiza wale wote ambao wanaendelea katika dhambi hizo. Wazazi hawa wanajua na wanaamini kwamba jahanum ipo. Kama tu vile imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, hivyo wao wanajua kwamba kwa imani wale wote ambao wanakataa kumwamini Kristo, wataingia jahanum. Kwa hivyo wao wana uoga kwamba watoto wao wako katika hatari ya kuingia humo jahanum.

### Wako na hasira kwa sababu ya dhambi za watoto wao.

Hasira ni jambo lingine ambalo liko katika mioyo ya wazazi ambao wameokoka kwa sababu watoto wao ni waovu. Hili ni jambo baya sana kwa sababu mtu akiwa na hasira, mara kwa mara yeye hujipata katika shida nyingi sana. Wazazi hawa wao hukasirishwa sana na dhambi za watoto wao. Wao wanakasirika kwa sababu wanawaona watoto wao wakimkana Mungu ambaye wao wenyewe kama wazazi wanajitahidi kila siku kuona kwamba wanamfurahisha. Wao wanakasirika kwa

sababu wanawaona watoto wao wakiharibu nafsi zao ambazo wao kama wazazi wamejitahidi sana kuona wanamjua Kristo, lakini wanakataa kuokoka. Pia wanakasirika sana kwamba wanaona watoto wao wakiyaharibu maisha yao katika tamaa za dhambi na kwamba wamesahau jinsi wazazi wao walivyojitahidi kuwafunza neno la Mungu na kuwaombea kusudi likiwa kwamba wamwamini Kristo. Wazazi hawa wanapoona mambo haya yote, wanajawa na hasira, maneno yao yanakuwa yenye hasira na kuwatazama watoto wao kwa hasira. Kwa sababu hii, watoto wao ambao wanafaa kuwa wenye kuwaletea furaha, wao wanageuka wenye kuwaletea huzuni mwingi sana.

**Wako na huzuni kwa sababu ya dhambi za watoto wao.**

Wazai hawa wanahuzunika sana kwa sababu ya uovu wa watoto wao. Ukweli kuhusu wokovu, huwafanya wao wahuzunike sana wakati wanapowaona watoto wao wakidharau na kukejeri utukufu wa Mungu na Kristo. Wakati wazazi hawa wao wanaishi maisha yao kwa ajili ya utukufu wa Mungu, wanahuzunika sana wakati wanawaona watoto wao wakiishi maisha yao katika anasa za dhambi. Upendo wao juu ya Mungu huwafanya waliye sana kwa ajili ya watoto wao ambao wanapenda dhambi, uovu na kumchukia Mungu ambaye kila kitu kizuri cha toka kwake.

**Huzuni huu mwingi unaletwa na mambo haya yafuatayo.**

a). Kwanza, huzuni huu mwingi huletwa wakati wazazi wanapowaza jinsi watoto wao walivyowaletea furaha wakati walikuwa watoto wadogo.

Ni jambo ambalo linawaletea huzuni mwingi sana wakati wanaona watoto wao ambao walikuwa na furaha pamoja na wao sasa wamegeuka na kuwa waasi dhidi ya Mungu na kuendelea kuyaharibu maisha yao. Wanahuzunika sana wanapokumbuka kwamba hawa watoto wao, utotoni mwao, waliwafurahia sana wazazi wao na kila wakati walipenda kuwa nao, lakini sana wamegeuka na kuwa watu wabaya sana ambao hawatii hata wazazi wao.

b). Pili, huzuni huu unaletwa na kushushwa mioyo kwa sababu yale walitarajia katika maisha ya watoto wao ni kinyume na jinsi watoto hao walivyo.

Biblia inasema kwamba, “Kilichotarajiwa kikikawia kuja, moyo huugua” (Mithali 13:12). Tumaini la wazazi hawa linapokatizwa kwa sababu ya uasi wa watoto wao, mioyo yao inaumia sana haswa kwa sababu ya maisha ya kiroho ya watoto wao. Wazai wanapokumbuka

jinsi watoto wao walivyokuwa wakisikiliza vizuri neno la Mungu na kuimba nyimbo mzuri za Mungu na jinsi walivyonekana katika utoto wao kuwa watu ambao wanampenda Mungu, na sasa kuwaona kwamba hawamdhamini Mungu kabisa katika maisha yao, ni jambo ambalo linawaletea huzuni mwingi sana.

c). Tatu, Wazazi pia wanahuzunika sana kuona kwamba watoto ambao waliwapenda sana wakati fulani, sasa watoto hao wanawachukia wazazi wao na wanapenda sana kuketi miongoni mwa vikundi vya waongo, walevi, wazinzi na wezi. Na kwamba vikundi hivi ndio vinawaletea furaha sana kuliko wazazi wao.

d). Nne, Wanahuzunik sana wakatia wanawatazama watoto wa wengine na kusema, "Asili yako mna kuzaliwa kwako kwatoka katika nchi ya Mkanaani; Mwamori alikuwa baba yako, na mama yako alikuwa Mhiti" (Ezekieli 16:3).

e).Tano, ni wahuzunisha wazazi haswa ikiwa wako na mtoto mmoja ambaye ni mwovu.

Huzuni mbaya sana unalinganishwa na kuombleza kwa ajili ya mtoto mmoja: "Ee binti wa watu wangu, ujivike nguo ya magunia, na kugaagaa katika majivu; fanya maombolezo, kama maombolezo ya uchungu mwingi; maana mwenye kuteka nyara atakuja juu yetu ghafula' (Yeremia 6:26). "..nao watamtazama yeye ambaye walimchoma; na watamwombolezea, kama vile mtu amwombolezeavyo mwanawe wa pekee' (Zekaria 12:10). Ninajua kwamba maandiko haya yanazungumzia wazazi ambao wanaomboleza kifo cha mtoto wao. Lakini ni huzuni sana kumwona mwana wako wa pekee akiwa ni mtu ambaye ni mwovu na hamchi Mungu, ambaye ni laana kwa wengi na anaendelea kuyaharibu maisha yake na nafsi yake. Ni jambo la kuhuzunisha tukijua kwamba huyu mtoto wazazi wake walitia bidi kuona kwamba anaenda katika njia za utakatifu. Wazazi wakiwaza juu ya upendo ambao walimwonyesha, jinsi walivyomshughulikia katika maisha yake, jinsi walivyomjali sana, maombi na kufunga kwao kwa ajili mtoto wao, haya mambo yote yanawahuzunisha sana.

f). Sita, wazazi wanahuzunika sana haswa ikiwa baba ni mchungaji katika kanisa.

Hili ni jambo la huzuni sana ikizingatiwa kwamba wewe mzazi ndiye huwa unawafundisha wengine na kuwahimiza wakati mambo yao ni magumu sana katika maisha. Wakati watoto wao wamekuwa wasumbufu, wewe ndiye huwa unaitwa kuomba nao na kuwasaidia katika kuleta suluhu. Lakini jambo la huzuni sana kwa mzazi huyu kwa

sababu sasa yeye ndiye ako katika hali hiyo. Hii inadhuru jinsi unapaswa kutekeleza majukumu yake kwa wengine. Kuna wale ambao wanaweza kusema, ikiwa yeye ameshindwa na wake, je atatusaidia kwa njia gani kama yeye mwenyewe ameshindwa kwake?

g). Saba, ni huzuni kwa wazazi haswa kwamba wawe walikuwa wamekusudia watoto wao watumike katika huduma na sasa wao ndio waasi.

Hili ni jambo la huzuni sana, kwa sababu wazazi walitaka watoto wao wakatumike na Mungu katika kanisa, na kwa sababu ya tamaa hii, walikuwa wamewapeleka masomo mazuri na kujitolea katika kila jambo ili wawasaidie watoto wao kumtumikia Mungu. Lakini sasa hawa watoto ndio wamegeuka na kuwa adui wa Mungu ambaye walikuwa wametayarishwa wamtumikia.

h). Nane,wazazi wanahuzunika sana haswa wakati wao ni wazee na watoto wao wanaanza kuwakosea heshima kama wazazi wao.

Biblia inasema kwamba, "Msikilize baba yako aliyekuzaa, Wala usimdharau mama yako akiwa mzee" (Mithali 23:22). Solomoni anasema kwamba siku za uzee ni siku za uovu (Mhubiri 12). Maisha ya uzee ni maisha ya taabu ambayo haiwezi kuondoka. Mtu akiwa mzee kwake kila kitu ni kama mzigo kwake. Kwa sababu wao wanazunika sana wakati wanaona kwamba watoto wao ni watu waovu na hawawajali.

# MAFUNDISHO JUU YA KUHUZUNIKA KWA SABABU YA WATOTO AMBAO NI WAOVU

## Edward Lawrence (1623-1695)

**Kwanza, ni dhambi kukosa kuendelea kutekeleza majukumu yako kwa sababu ya uovu wa watoto wako.**

Ikiwa wewe utakufa moyo na kuacha kutekeleza majukumu ambayo Mungu anataka utekeleza kwa sababu mtoto au watoto wamekuwa waovu, basi ni kuonyesha kwamba tegemeo lako, si Kristo bali ni watoto wenyewe. Kumbuka maneno ya Joabu kwa Daudi wakati Daudi alikuwa anahuzunika kwa sababu mtoto wake Absolomu: "kwa kuwa unapenda wakuchukiao, na unawachukia wakupendao. Maana umetangaza leo ya kuwa wakuu na watumishi wako si kitu kwako; maana leo nimetambua

hivi; kama Absolomu angeliishi, na sisi sote tungalikufa leo, ingalikuwa vyema machoni pako" (2 Samweli 19:6). Kwa hivyo ninakuambia leo kwamba ikiwa unakufa moyo kwa sababu ya uovu watoto wako, basi ni wazi kwamba Mungu na Kristo hachukii nafasi ya kwanza katika moyo wako.

**Pili, Kumbuka kwamba hili ni jambo amablo mara kwa mara linawakumba watoto wa Mungu.**

Hufai kuwaza kwamba wewe ndiye mzazi ambaya ameokoka wa kwanza ambaye watoto wake ni waovu, au kwamba hili ni jambo geni kwako. Usiwaza kwamba Mungu hakupendi ama kuna jambo baya sana ambalo umelifanya na sasa Mungu analipiza kisasa. Usilie kwa kusema, "Angalieni, mtazame Kama kuna majonzi yangu yoyote mfano wa majonzi yangu, Niliyetendwa mimi, Ambayo Bwana amenihuzunisha kwa hayo siku ya hasira yake iwakayo" (Maombolezi 1:12). Kumbuka kwamba huzuni huu ni kawaida kwa wale ambao wameokoka.

**Tatu, Kumbuka kwamba kuna jambo kubwa sana katika maisha yako ambalo lingekufanyikia kuliko hili.**

Nitakuonyesha mambo matatu ambayo yangekunyikia makubwa kuliko hili la mtoto au watoto wako kuwa waasi dhidi ya Mungu. Kwanza, wewe wenywe huenda ungekuwa mwovu sana. Na kwamba kama Mungu agekuhukumu milele, hilo lingekuwa jambo baya sana katika maisha yako. Pili, huenda ungekuwa na mke au mume ambaye hajaokoka na hili lingekuwa jambo la kukuhuzunisha sana kila wakati. Biblia inasema hivi kuhusu mke au mume ambaye hajaokoka, "Mwana mpumbavu ni msiba kwa babaye. Na ugomvi wa mke kama kutona-tona daima" (Mithali 19:13). Hii ni kama mvua kunyesha katika nyumba kila wakati na maji hayo kuharibu vitu vya nyumba na kufanya wale ambao wanakaa nyumba hio kukosa Amani ya kuishi humo. Kwa sababu mke au mume wako ako karibu nawe na kwamba ameokoa, ni jambo la faraja sana kuliko kuwa na mtoto mwovu. Tatu, Mungu huenda angeacha watoto wako wote waangamia katika dhambi. Lakini ikiwa uko na mtoto mmoja ambaye ameokoka, shukuru Mungu hiyo ni furaha yako na wacha kuomboleza sana juu ya yule ambaye hajaokoka.

**Nne, hakikisha kwamba huzuni wako unaongozwa na Biblia ili usije ukamkasirisha Mungu, kuchafua nafsi yako na kuumiza dhamira yako kwa sababu kuhuzunika ni dhambi.**

Kuna mambo mawili hapa ya kuzingatia ili tusitende dhambi dhidi ya Mungu. Kwanza, ikiwa ni kuhuzunika, huzunika kwa sababu ya dhambni zao dhidi ya Mungu na wala si kwa sababu wewe unaibika kuwa na watoto ambao hawajokoka. Kwa njia hii, itadhihirika kwamba unapendezwa kuona kwamba Mungu anatukuzwa na watoto wako wanaokoka na si kwa sababu ya heshima kwako kutoka kwa ulimwengu. Ni ukweli kwamba katika kuomboleza kwa wazazi mara mingi huzuni wao ni kwa vitu vya ulimwengu na si kwa utukufu wa Mungu na uokovu wa nafsi ya mtoto wake. Pili, hakikisha kwamba kuomboleza kwako hakudhuru mwili na afya yako. Mungu anataka tuhuzunika sana kwa ajili ya dhambi zetu wenyewe na si kwanza ajili ya dhambi za watoto wetu. Hatufai kuiharibu miili yetu katika huzuni kwa sababu miili yetu ni hekalu la Roho Mtakatifu. Ukweli ni kwamba huzuni ambao unamletea Mungu utukufu ni mzuri na huwa haudhuru afya au mwill ya mtu. Neema kila wakati ni rafiki na wala si adui wetu. Kwa hivyo katika maombolezi usije ukapuuza kumtukuza Mungu na kumtumikia katika kanisa lake. Usije ukawafanya watoto kuhuznika au mke au mume wako kuhuzunika kwa sababu ya huzuni wako. Usiwaongoze wengine katika dhambi kwa sababu ya kukosa kufuata mafundisho ya Biblia kuhusu huzuni.

**Tano, Kumbuka kuhakikisha kwamba unamwomba Mungu akupatia nguvu katika huzuni juu ya watoto wako.**

Ninasema hivi kwa sabaabu, katika hali kama hii, unahitaji hekima, Imani, tumaini, upendo, unyenyekevu na uvumilivu ili uweze kuendelea katika maisha yako vyema. Unahitaji neema ya Mungu na upendo wa Kristo katika wakati wa huzuni wako. Kwa nguvu za Kristo, utawezeshwa kuendelea vyema maishani mwako na wakati huo huo ukimtukuza Kristo. Ukweli ni kwamba kwa wakristo, ukubwa wa majaribu ndivyo mkristo anavyofaidika kiroho.

**Sita, Kumbuka kwamba Mungu huwa anatukuzwa katika kila jambo.**

Mungu atatukuzwa katika hali yoyote ambayo mtoto wako atakuwa. Kila kitu kinafanyika kwa utukufu wa Mungu. Yesu Kristo alitoka kwa Mungu na anafanya kazi ya kutuakilisha mbele za Mungu akiwa mtumishi wa Mungu na kwa utukufu wa Mungu. Malaika wote na watakatifu wote milele tutamheshimu, kumtamani, kumpenda na kumsifu.

Mungu Baba, Mungu Mwana na Mungu Roho Mtakataifu ako pamoja nawe na milele Mungu atatukuzwa kwa kukubariki na kukuleta katika utukufu. Ni ukweli uko na mtoto mbaya lakini pia zaidi uko na Mungu mwema. Kumbuka dhambi zako zote zitaondolewa na kusamehewa, wewe utakamilishwa na mwili wako na nafsi yako vitaletwa katika utukufu. Kwa hivyo uasi wa mtoto wako ni kitu kidogo sana ambacho hakifai kukuhuhuzunisha kiwango kwamba umtendee Mungu dhambi.

**Saba, Kumbuka kwamba shida hii ni ya muda mfupi tu.**

Hakuna kitu kingine ambacho kinaweza kutupatia tumaini la kweli wakati wa shida ya watoto wetu kutoamini kama kujua kwamba shida hiyo ni ya muda tu. Hatutakuwa wenye huzuni siku zote, ikiwa tumemwamini Kristo, huzuni wetu ni wa muda tu kwa sababu Mungu atatuingiza katika utukufu wa milele mahali ambapo hakuna kilio au huzuni. Pia kumbuka kwamba kuna wale ambao pia wamekuwa na watoto waovu lakini baada ya muda watoto hao walikoka. Hakuna furaha ya kweli kujua kwamba siku moja tutaketi na Kristo na huzuni wa aina yoyote utaisha.

# KUWALEA WATOTO NI FURSA KUBWA YA KUUSHUDIA ULIMWENGU KUHUSU KRISTO

## David Martyn Lloyd-Jones (1899-1981)

Paulo akimwandikia Timotheo anamwambia kwamba wakati unakuja ambapo wengi wataiacha imani ya kweli. Anasema kwamba moja wapo wa ishara wakati huo ni kwamba watoto watakosa kuwatii wazazi wao (2 Timotheo 3:2). Unapotazama yale ambayo yanaendelea katika nchi nyingi, ukweli ni kwamba watu wamekosa kumtii Mungu. Hili ni jambo ambalo kila serikali inapaswa kufahamu. Uovu wa ukosefu wa kutii sheria ni kwa sababu watu hawajafunzwa kutii mamlaka kwa sababu wengi wao hata hawatii wazazi wao. Shida kubwa ya serikali zetu ni kwamba wale ambao wako uongozini, hawatii Biblia. Wao wanawaza kwamba watafaulu katika kuondoa dhambi. Kuwaza hivi ni

kujidanganya kabisa. Wengi hawatii sheria kwa sababu wao ni wenye dhambi. Ikiwa serikali inatarajia kuona watu wake wakitii sheria, ni lazima dhambi ishughulikiwa kabisa. Hili ndilo jambo ambalo linaelezwa katika Waefeso 6:1-4. Unapotazama ulimwenguni kote, utapata kwamba wakati ambapo kuwekuwepo utulivu katika nchi fulani fulani, ni wakati ambapo kumekuwepo na msingi bora ya Biblia. Ni wakati ambapo kuna wengi walizingatia mafundisho ya Biblia na kuhakikisha kwamba wanawahimiza wengi kutii kile ambacho Biblia inasema. Hii shida ya ukose wa nidhamu miongoni mwa watoto na vijana, hikuwa hivi katika miaka minigi imepita. Hii ni kwa sababu wengi katika manyumba zao, walifundisha na kuzingatia mafundisho ya Biblia. Lakini sasa tunaona kwamba uovu umerudi na uko pamoja nasi leo, wengi haswa watoto wetu hawataki kuishi chini ya mamlaka.

Kwa hivyo tunapaswa kuzingatia sana maneno ya Paulo katika 2 Timotheo 3:2. Ninaamini kwamba wazazi ambao wameokoka na watoto wao, jamii ambazo zimeokoka zote tuko na fursa ya kushuhudia Kristo leo kwa ulimwengu wote kwa kuwa tofauti na jinsi wengi walivyo. Tunaweza kuwa mashahidi wakweli kwa kuzingatia nidhamu, kutii sheria za nchi na kuwa watu wa amani. Ni lazima kuwe na uhusiani mwema kati ya watoto na wazazi wao. Sisi ndio Mungu ameweka kuleta nuru yake katika ulimwengu huu na kuhakikisha kwamba neno la Mungu linafundishwa vyema kwa wote. Kwa hivyo kila mmoja wetu ajitolea kuhakikisha kwamba tunaleta tofauti ambayo ni kuishi maisha yetu kulingana na mafundisho ya neno la Mungu.